MAZINGIRA: Nyasi, zaidi ya 1200 m kutoka usawa wa bahari

HISTORIA ASILIA: Madume yanaita kutoka uoto uliopo juu ya maji kwenye maeneo yanayozunguka maji

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Savana kwenye maeneo ya juu ya kati ya Tanzania, kuanzia mharara wa Tao la Mashariki kuelekea magharibi

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Uhehe, Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: < 2400 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini

Hyperolius kihangensis (Schlötter & Westergaard, 1999)
Kihanga Reed Frog



M. Menegon

SVL: ♂ 16 - 19 mm; ♀ 23 - 26 mm

DESCRIPTION: A small *Hyperolius*. The dorsum is mottled brown and gray with small dark spots, a broad light band across the lower back and a small white dot on each heel. Some individuals have an hourglass pattern on the dorsum. Toes and fingers are yellowish to reddish. The ventral surface is yellow in males and reddish in females.

SIMILAR SPECIES: The dorsal pattern of this species is distinctive.

HABITAT: Swamps in montane forest

NATURAL HISTORY: The natural history of this species is not well known.

CALL: A series of quiet clicks

DISTRIBUTION IN THE EACF: Known only from the Luhega Forest in the Uzungwa Mountains

TYPE LOCALITY: Uzungwa Scarp Forest Reserve, Uzungwa Mountains, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: 1740 m

CONSERVATION STATUS: Endangered

UREFU WA MWILI: ♂ 16 - 19 mm; ♀ 23 - 26 mm

MAELEZO: *Hyperolius* huyu ni mdogo. Sehemu ya mgongoni ina madoa ya kahawia na kijivu; aidha ina madoa madogo meusi, mstari mpana wenye rangi iliyofifia kutoka upande mmoja hadi mwingine wa sehemu ya chini ya mgongo na doa moja dogo jeupe kwenye kila wayo. Baadhi ya vyura wana umbo la "V" mbili zinazogusana moja ikiwa chini juu kwenye sehemu ya juu. Vidole vya miguu na mikononi ni njano njano hadi rangi nyekundu nyekundu. Sehemu ya chini ya madume ni njano na ya majike ni nyekundu nyekundu.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Mpangilio wa sehemu ya juu unatofautisha spishi hii na nyingine kwenye jenasi.

MAZINGIRA: Vinamasi kwenye misitu iliyopo zaidi ya 1200 m kutoka usawa wa bahari

HISTORIA ASILIA: Historia asilia ya spishi hii haijulikani vizuri.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Misitu ya Luhega ya Milima ya Udzungwa tu

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Miteremko ya Hifadhi ya Misitu ya Milima ya Udzungwa, Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: 1740 m

HALI YA UHIFADHI: Spishi iko hatarini



Hyperolius mariae (Barbour and Loveridge, 1928)

Mary's Reed Frog



J. Vonesh

SVL: ♂ & ♀ < 25 mm

DESCRIPTION: A small *Hyperolius* with a short snout. The dorsum is pale tan with a dark blueish-black band low on each side. Black canthal stripes are usually present, sometimes extending over the eye to the base of the arm. The tympanum is not visible. The hands, feet and ventral surface are reddish. The toes are nearly fully webbed.

SIMILAR SPECIES: The dorsal markings are distinct. *H. mariae* is part of the *Hyperolius viridiflavus* superspecies (see discussion under *H. glandicolor*).

Pickersgill (2007) considers coastal and island populations to be *Hyperolius viridiflavus renschi*, and only the populations further inland to be *H.v. mariae*.

HABITAT: Swamps, rivers and lakes in savanna, grassland and shrubland.

NATURAL HISTORY: Males call from exposed sites on vegetation near water. Clutches of around 330 small black and white eggs are deposited in open water. Tadpoles hatch after about six days.

CALL: Schiøtz (1999) describes the call as “a fast series of high-pitched clicks.”

DISTRIBUTION IN THE EACF: Coastal areas of southern Kenya and Tanzania, inland to Mikumi National Park and the islands of Pemba, Zanzibar and Mafia.

TYPE LOCALITY: East Usambara Mountains, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: < 1400 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ & ♀ < 25 mm

MAELEZO: *Hyperolius* huyu ni mdogo na ana pua fupi. Sehemu ya juu ni hudhurungi iliyofifia na kuna mstari bluu nyeusi chini ya kila upande. Kwa kawaida, kuna mistari kati ya pua na macho, na wakati mwingine inatoka juu ya jicho hadi mwanzoni mwa mkono. Kiwambo cha sikio hakionekani. Viganja, nyayo na sehemu ya chini vina rangi nyekundu nyekundu. Vidole vya miguuni vina utando.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Alama kwenye sehemu ya juu zinaitofautisha spishi hii na nyingine kwenye jenasi. *H. marie* ni sehemu ya spishi ya juu kabisa ya *Hyperolius viridiflavus* (rejea taarifa za *H. glandicolor*). Msimamo wa Pickersgill (2007) ni kwamba spishi za pwani na visiwani ni *Hyperolius viridiflavus renschi* na spishi za bara tu ni *H. v. mariae*.

MAZINGIRA: Vinamisi, mito na maziwa kwenye maeneo ya savana, nyika na vichaka.


HISTORIA ASILIA: Madume yanaita kutoka sehemu wazi kwenye uoto karibu na maji. Makundi ya mayai madogo meusi na meupe takribani 330 yanatagwa kwenye maji. Viluwilwi vinatolewa baada ya takribani siku sita.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Maeneo ya pwani ya kusini mwa Kenya na Tanzania, bara hadi Hifadhi ya Taifa ya Mikumi na visiwa vya Pemba, Zanzibar na Mafia.

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Milima ya Usambara Mashariki, Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI:
< 1400 m

HALI YA UHIFADHI: Spishi haiko hatarini



Hyperolius minutissimus (Schiøtz, 1975)

Tiny Reed Frog, Dwarf Reed Frog



M. Menegon

SVL: ♂ 12 – 17 mm; ♀ 18 – 24 mm

DESCRIPTION: A small *Hyperolius* with a brown dorsum and broad light canthal and dorsolateral stripes that may be green or yellow. Some individuals also have light spots on the legs and dorsum.

SIMILAR SPECIES: The tiny males may be confused with *H. pictus* metamorphs, but the latter typically have three distinct lines on the dorsum which *H. minutissimus* lacks. *H. minutissimus* is similar to *H. spinigularis*, but *H. minutissimus* lacks blue coloration and the males are substantially smaller than in *H. spinigularis*.

HABITAT: Open high-elevation grasslands and forest clearings

NATURAL HISTORY: Breeds in temporary pools in grasslands.

CALL: Described by Schiøtz (1999) as “a fast series of quiet, unmelodic clicks.”

DISTRIBUTION IN THE EACF: Udzungwa Mountains and the Southern Highlands

TYPE LOCALITY: 10 miles west of Njombe, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: Above 1800 m

CONSERVATION STATUS: Vulnerable

UREFU WA MWILI: ♂ 12 – 17 mm; ♀ 18 – 24 mm

MAELEZO: *Hyperolius* huyu ni mdogo na sehemu ya juu ni kahawia. Aidha, ana mistari mipana kati ya pua na macho, mgongoni na pembeni ambayo ni kijani au njano. Baadhi ya vyura wana madoa yaliyofifia kwenye miguu na sehemu ya juu.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Ni rahisi kuchanganya madume yake madogo sana na *H. pictus* anayetoka kupata umbile la chura mzima, ana mistari mitatu sehemu ya juu ambayo *Hyperolius minutissimus* hana. Aidha, *Hyperolius minutissimus* anafanana na *H. spinigularis* lakini *Hyperolius minutissimus* haina rangi ya bluu na madume yake ni madogo zaidi kuliko ya *H. spinigularis*.

MAZINGIRA: Nyika zilizo wazi kwenye miinuko ya juu.

HISTORIA ASILIA: Spishi inazaliana kwenye madimbwi ya muda nyikani.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Milima ya Udzungwa na ya Nyanda za Kusini

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Maili 10 magharibi mwa Njombe, Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: > 1800 m

HALI YA UHIFADHI: Spishi inaweza kuathiriwa



Hyperolius mitchelli (Loveridge, 1953)

Mitchell's Reed Frog



E. Harper

SVL: ♂ 23 – 27 mm; ♀ 25 – 32 mm

DESCRIPTION: The dorsum is orange to brown, often with small dark spots especially in young individuals. Light canthal and dorsolateral stripes are always present and are usually outlined in black, and in some cases yellow as well. The dorsolateral stripes extend midway down the dorsum and in some individuals reach the groin. A light spot is present on each heel. The ventral surface of males may be yellow or orange, but in females is typically orange. Males have a yellow gular flap.

SIMILAR SPECIES: *H. mitchelli* can be distinguished from *H. puncticulatus* by the light spots on the heels.

HABITAT: Dry and moist forest, also found in degraded habitat including gardens and low-intensity agricultural land.

NATURAL HISTORY: Clutches of 50 – 100 eggs are laid on vegetation over water. Tadpoles hatch after five or six days.

CALL: Males call from vegetation over streams or ponds. Schiøtz (1999) describes the call as “an irregular series of screams.”

DISTRIBUTION IN THE EACF: Eastern Tanzania including the foothills of the Udzungwa, Ulunguru, Malundwe, Mahenge, Nguu, Nguru and Usambara Mountains

TYPE LOCALITY: Mtimbuka, Lake Nyasa, Malawi

ELEVATIONAL RANGE: up to 1200 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ 23 – 27 mm; ♀ 25 – 32 mm

MAELEZO: Sehemu ya juu ni njano hadi kahawia na mara nyingi kuna madoa madogo meusi kwenye vyura wadogo. Mistari ya mgongoni na pembeni ipo wakati wote na mara nyingi inazungukwa na rangi nyeusi na wakati mwingine rangi ya njano. Kwenye baadhi ya vyura, mistari ya mgongoni na pembeni inapita kwenye nusu ya sehemu ya juu hadi kwenye kinena. Kuna doa dogo lenye rangi iliyofifia kwenye wayo. Sehemu ya chini ya madume ni njano au rangi ya machungwa lakini kwenye majike ni ya machungwa tu. Madume yana kipande cha ngozi njano chini ya koo.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Madoa yenye rangi iliyofifia kwenye visingo *H. mitchelli* na *H. puncticulatus*.

MAZINGIRA: Misitu kame na yenye mvua, mazingira yaliyoharibiwa, bustani na maeneo ya kilimo yasiyolimwa sana.


HISTORIA ASILIA: Makundi yenye mayai 50 - 100 yanatagwa kwenye uoto juu ya maji. Viluwiluwi vinatolewa baada ya siku tano au sita.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Tanzania Mashariki pamoja na milima midogo ya Milima ya Usambara Magharibi, Usambara Mashariki, Nguu, Nguru, Mahenge, Uluguru, Malundwe, Udzungwa

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Mtimbuka, Ziwa Nyasa, Malawi

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: < 1200 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Hyperolius parkeri (Loveridge, 1933)

Parker's Reed Frog, Brown-or-green Sedge Frog



E. Harper

SVL: 21 – 28 mm

DESCRIPTION: A small *Hyperolius* with an elongate body and pointed snout. Unlike other *Hyperolius spp.*, the males are larger than the females. Dorsal color may be brown or green in males while females are green. Both have distinct light dorsolateral bands outlined with small dark spots. Toes are extensively webbed. Males in breeding condition have small black spines on the undersides of the legs.

SIMILAR SPECIES: Not easily confused with other species.

HABITAT: Coastal savannas, humid woodlands and degraded forest

NATURAL HISTORY: Clutches of 36 – 110 unpigmented eggs are attached to vegetation in marshes above the water's surface. The tadpoles are unknown.

CALL: Males call from concealed positions on vegetation over streams or ponds and call without elevating the head. Schiøtz (1999) describes the call as "a high-pitched trill" approximately 1.5 seconds in duration.

DISTRIBUTION IN THE EACF: Coastal areas of Kenya and Tanzania inland to the Kilombero flood plain, also found on the island of Zanzibar

TYPE LOCALITY: Mogoni swamp, south of Dar es Salaam, Usaramo, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: < 1000 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: 21 – 28 mm

MAELEZO: *Hyperolius* huyu ni mdogo, ana mwili mrefu na pua iliyochongoka. Tofauti na *Hyperolius spp.* wengine, madume ni makubwa kuliko majike. Sehemu ya juu ya madume ni kahawia au kijani wakati ya majike ni kijani. Madume na majike yana mistari iliyofifia mgongoni na pembeni, iliyozungukwa na madoa madogo meusi. Vidole vya mguuni vina utando mwingi. Madume yanapokuwa kwenye msimu wa kupandana yana miiba midogo mieusi sehemu ya chini ya miguu.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Siyo rahisi kuichanganya na spishi zingine

MAZINGIRA: Savana ya pwani, miombo yenye unyevu na misitu iliyoharibiwa


HISTORIA ASILIA: Makundi ya mayai 36 - 110 yasiyokuwa na rangi yanagandishwa kwenye uoto juu ya maji, maeneo ya vinamasi. Hakuna taarifa za viluwilwi.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Pwani ya Kenya na Tanzania hadi bara kwenye Bonde la Kilombero, na kisiwa cha Zanzibar.

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Kinamasi cha Mogoni, kusini mwa Dar es Salaam, Uzaramo, Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: < 1000 m

HALI YA UHIFDHI: Haiko hatarini



Hyperolius pictus (Ahl, 1931)

Variable Reed Frog, Ahl's Painted Reed Frog, Variable Montane Sedge Frog



M. Menegon

SVL: ♂ & ♀ 23 – 31 mm

DESCRIPTION: A medium-sized *Hyperolius* with short legs and variable dorsal patterns. Individuals may be brown with cream or green canthal, dorsolateral and middorsal stripes. Green spots may be present on the arms and legs. Some individuals may be green without brown markings. The ventral surface and insides of the legs are yellow. Juveniles are typically brown with three green dorsal stripes. There is a small amount of webbing on the fingers. Toes are approximately ½ webbed.

SIMILAR SPECIES: Some individuals have color patterns similar to morphs of *H. minutissimus*.

HABITAT: High elevation grasslands. Tolerates a moderate degree of habitat modification and can be found in some agricultural areas.

NATURAL HISTORY: Breeds in streams and permanent and temporary pools. Females lay groups of 60 – 90 eggs on vegetation above water.

CALL: Schiøtz (1999) describes the call as “alternating slow and fast unmelodic creaks, uttered with rather long intervals.”

DISTRIBUTION IN THE EACF: Udzungwa Mountains, Southern Highlands, and Ufipa Plateau. Records from the East Usambaras and Kilombero Valley are unconfirmed.

TYPE LOCALITY: “Krater des Ngori-See’s” Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: Approximately 1400 – 2000 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ & ♀ 23 – 31 mm

MAELEZO: Chura huyu ni *Hyperolius* mwenye saizi ya kati, miguu mifupi na mpangilio wa sehemu ya juu unaotofautiana. Baadhi ya vyura ni kahawia na wana mistari kati ya pua na macho, mgongoni na pembeni na katikati ya sehemu ya juu, yenye rangi ya malai au kijani. Wakati mwingine panakuwa na madoa ya kijani mikononi na miguuni. Baadhi ya vyura wanaweza kuwa kijani bila alama za kahawia. Sehemu ya chini na chini ya miguu ni manjano. Vyura wadogo ni kahawia na wana mistari mitatu ya kijani sehemu ya juu. Kuna utando kidogo kwenye vidole vya mikononi. Vidole vya miguuni vina utando kwenye ½ ya sehemu.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Baadhi ya vyura wana mpangilio wa rangi unaofanana na vyura wa *H. minutissimus* katika hatua mbalimbali.

MAZINGIRA: Nyika za miinuko ya juu. Inavumilia mabadiliko kiasi ya mazingira na inapatikana pia kwenye maeneo ya kilimo.


HISTORIA ASILIA: Inazaliana kwenye vijito na mabwawa ya muda na ya kudumu. Majike yanataga makundi ya mayai 60-90 kwenye uoto juu ya maji.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Milima ya Udzungwa, Nyanda za Kusini na Uwanda wa Ufipa. Aidha, kuna taarifa ambazo hazijathibitishwa za spishi kupatikana Usambara Mashariki na Bonde la Kilombero.

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: “Krater des Ngori-See’s” Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: takribani 1400 – 2000 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Hyperolius pseudargus (Schiztz & Westergaard, 1999)
Mette's Reed Frog



M. Menegon

SVL: ♂ 32 – 35 mm

DESCRIPTION: A green *Hyperolius* with narrow yellow canthal and dorsolateral stripes, although stripes may be less distinct in some individuals than others. Most individuals have small yellow dots on the dorsum. The upper eyelid is yellow or slightly reddish. The ventral surface is yellow. Toes and fingers are yellow-green and have a small amount of webbing at the base. The throat of males is yellow-green, but the vocal sac appears blue when males are calling.

SIMILAR SPECIES: Similar coloration to

male *H. argus*, but *H. pseudargus* has less extensive webbing on the toes.

HABITAT: High elevation grasslands and degraded habitats including open farmland, pastures, gardens and former forest.

NATURAL HISTORY: Breed in permanent and temporary marshes, pools and ponds. Males call while perched on emergent and floating vegetation.

CALL: Schiztz (1999) describes the call as “a fast series of very loud, harsh clicks in a somewhat accelerating rhythm, about 10 per second and decelerating towards the end.”

DISTRIBUTION IN THE EACF: Udzungwa Mountains and Njombe in the Southern Highlands

TYPE LOCALITY: Udzungwa Mountains, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: 1500 – 1850 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ 32 – 35 mm

MAELEZO: *Hyperolius* huyu ana mistari miembamba na kijani kati ya pua na macho, mgongoni na pembeni, ingawa mistari huenda haionekani sana katika baadhi ya vyura. Idadi kubwa ya vyura wana madoa madogo ya njano kwenye sehemu ya juu. Kigubiko cha jicho la juu ni njano au chekundu kidogo. Sehemu ya chini ni njano. Vidole vya miguuni na mikononi ni njano kijani na vina utando kidogo mwanzoni. Koo la majike ni njano kijani lakini kifuko cha sauti kinaonekana bluu madume yanapoita.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Madume yana rangi inayofanana na ya *H. argus*, lakini *H. pseudargus* hana utando mwingi kwenye vidole vya miguuni.

MAZINGIRA: Nyika kwenye miinuko ya juu na mazingira yaliyoharibiwa, pamoja na maeneo ya kilimo, malisho ya wanyama, bustani na mahali palipokuwa na misitu awali.


HISTORIA ASILIA: Inazaliana kwenye vinamasi vya muda na vya kudumu na madimbwi. Madume yanaita yakiwa kwenye uoto ulio juu ya maji au unaoelea.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Milima ya Udzungwa na Njombe, Nyanda za juu za Kusini

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Milima ya Udzungwa, Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: 1500 – 1850 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Hyperolius puncticulatus (Pfeffer, 1893)
Spotted Reed Frog



E. Harper

SVL: ♂ 21 – 29 mm; ♀ 30– 37 mm

DESCRIPTION: Color pattern is highly variable. The dorsum is typically orange with light canthal and dorsolateral stripes that are often outlined in black. The dorsolateral stripes extend almost to the vent in some individuals, and continue as a series of spots in others. One or two spots may also be present along the middle of the dorsum. An alternate morph consists of orange individuals with black reticulations, although this pattern is less common. In a third morph, the dorsum is covered in yellow spots

outlined in black, with very little orange showing through. The throat of males is orange and the ventral surface is yellow. Males have a yellow gular flap.

SIMILAR SPECIES: *H. puncticulatus* is similar to *H. mitchelli* in size and coloration, but lacks the light spots on the heels. Pickersgill (2007) considers this species to be *H. substriatus*.

HABITAT: Dry and moist forest, savanna and shrubland. Tolerates some degree of habitat alteration.

NATURAL HISTORY: Males call while perched on emergent vegetation in permanent and temporary pools. Females attach masses of pigmented eggs to vegetation above water. Clutch size has not been recorded, and the tadpoles have not been described.

CALL: The call is a series of short high-pitched clicks.

DISTRIBUTION IN THE EACF: Eastern Tanzania

TYPE LOCALITY: “Magrotto bei Tanga,” East Usambaras, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: 0 - 2000 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ 21 – 29 mm; ♀ 30 – 37 mm

MAELEZO: Sehemu ya juu ina rangi ya machungwa na mistari iliyofifia kati ya pua na macho, mgongoni na pembeni ambayo ni mieusi mara nyingi. Mistari ya mgongoni na pembeni inafika karibu na tundu la kutolea haja na kutoa na kupokelea mbegu za uzazi katika baadhi ya vyura na baada ya hapo kuna madoa. Inawezekana kukawa na doa moja au mawili katikati ya mgongo kwenye vyura wengine. Kuna mpangilio mwingine wa rangi; baadhi ya vyura ni njano na wana wavu mweusi lakini mpangilio huu haupo sana. Koo la madume lina rangi ya machungwa na sehemu ya chini ni njano. Madume yana kipande cha ngozi chini ya koo.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Spishi hii inafanana na *H. mitchelli* kwa saizi na rangi, lakini haina madoa kwenye kisigino. Maoni ya Pickersgill (2007) ni kwamba spishi hii ni *H. substriatus*.

MAZINGIRA: Mimitu kame na yenye mvua, savana, maeneo ya vichaka. Inavumilia mazingira yaliyobadilika kiasi.


HISTORIA ASILIA: Madume yanaita yanapokuwa kwenye uoto uliopo juu ya maji kwenye madimbwi ya muda na ya kudumu. Majike yanataga na kugandisha mayai yenye rangi kwenye uoto juu ya maji. Hakuna taarifa juu ya ukubwa wa makundi ya mayai na hakuna maelezo juu ya viluwiluwi.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Mashariki Tanzania

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: “Magrotto bei Tanga,” Usambara Mashariki, Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: 0 - 2000 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Hyperolius pusillus (Cope, 1862)

Translucent Tree Frog, Water Lily Reed Frog



R. Drewes

SVL: ♂ & ♀ < 25 mm

DESCRIPTION: A small translucent *Hyperolius* with variable dorsal patterns. The dorsum is typically green, but may also appear clear or yellowish. There are dark canthal stripes and often dark dots on the dorsum. Many individuals have light dorsolateral stripes. The tibia is approximately ½ SVL. Fingers are webbed at the base and the toes are extensively webbed. Toes and fingers can be yellow, orange or green. The ventrum has a transparent patch through which the internal organs are visible.

SIMILAR SPECIES: Not easily confused with other species.

HABITAT: It is common and abundant in swampy areas with vegetation in savannas, shrubland, and grassland habitat.

NATURAL HISTORY: Males call while perched on floating vegetation. Breeding takes place in a wide range of aquatic habitat types.

CALL: Schiøtz (1999) describes the call as “a fast series of high-pitched screams.”

TYPE LOCALITY: KwaZulu-Natal, Republic of South Africa

DISTRIBUTION IN THE EACF: Coastal Kenya and Tanzania, including Mafia and Songo Songo islands.

ELEVATIONAL RANGE: < 800 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ & ♀ < 25 mm

MAELEZO: *Hyperolius* huyu ni mdogo, angavu na ana mpangilio unaotofautiana sehemu ya juu. Kwa kawaida, sehemu ya juu ni kijani lakini inaweza pia kuwa njano. Aidha, kuna mistari kati ya pua na macho na madoa meusi sehemu ya juu. Vyura wengi wana mistari mgongoni na pembeni. Miguu ni takribani ½ ya SVL. Vidole vya mikononi vina utando mwanzoni na vidole vya miguuni vina utando mwingi. Vidole vya miguuni na mikononi vinaweza kuwa njano, rangi ya machungwa au kijani. Sehemu ya chini ina doa angavu linaloweza kuona ogani za ndani.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Sio rahisi kuchanganya spishi hii na zingine.

MAZINGIRA: Inapatikana kwa wingi kwenye vinamasi vyenye uoto, kwenye savanna, maeneo ya vichaka na nyika.


HISTORIA ASILIA: Madume yanaita yanapokuwa kwenye uoto unaoelea. Spishi inazaliana kwenye aina nyingi za mazingira yenye maji

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: KwaZulu-Natal, Jamhuri ya Afrika ya Kusini

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Pwani ya Kenya na Tanzania, pamoja na visiwa vya Mafia na Songo Songo.

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: < 800 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Hyperolius reesi (Schlötter, 1982)

Magombero Reed Frog



A. Schlötter

SVL: ♂ 22 mm; ♀ 26 mm

DESCRIPTION: A medium-sized *Hyperolius* with long legs and large dark eyes. The dorsum is yellow-brown to pale green. On the sides are distinct dark and light vertical stripes. In a few individuals the lighter stripes are more variable and may appear as dots or be completely absent. The nostrils are typically outlined in black. The ventral surface is white. Toes are pinkish or yellow and are partially webbed. There are small dark dots on the hands and feet. The throat is yellow in males and white in females.

SIMILAR SPECIES: Part of the *Hyperolius viridiflavus* complex. Similar to *H. mariae*, but the vertical stripes on the sides are distinctive.

HABITAT: Found in a wide variety of habitat types including forest, grasslands, shrubland and savanna.

NATURAL HISTORY: Breeding takes place in nearly any type of aquatic habitat that has emergent vegetation including lakes, ponds, streams and swamps.

CALL: Schlötter (1982) described the call as “a fast series of clicks”

TYPE LOCALITY: Magombero Forest, Kilombero-Rufiji area, Tanzania

DISTRIBUTION IN THE EACF: Udzungwa Mountains and Kilombero floodplains

TYPE LOCALITY: Kilombero-Rufiji region, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: 200 – 900 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ 22 mm; ♀ 26 mm

MAELEZO: *Hyperolius* huyu ana saizi ya kati, miguu mirefu na macho makubwa meusi. Sehemu ya juu ni njano kahawia hadi kijani kilichofifia. Pembeni kuna mistari wima mieusi inayoonekana. Vyura wachache wana mistari iliyofifia na inayotofautiana na wakati mwingine inaonekana kama madoa au inakuwa haipo kabisa. Mashimo ya pua yamezungushiwa rangi nyeusi pembeni. Vidole vya miguuni ni rangi ya waridi au njano na vina utando kiasi. Kuna madoa madogo meusi kwenye mikono na miguu. Koo la madume ni njano na la majike ni jeupe.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Spishi hii ni sehemu ya mchanganyiko wa spishi wa *Hyperolius vidiflavus*. Inafanana na *H. mariae* lakini ina mistari wima pembeni.

MAZINGIRA: Inapatikana kwenye aina mbalimbali za mazingira pamoja na misitu, nyika, vichaka na savana.

HISTORIA ASILIA: Inazaliana karibu kwenye kila aina ya mazingira ya maji ambayo yana uoto uliopo juu ya maji; mazingira haya ni maziwa, madimbwi, vijito na vinamasi.

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Misitu ya Magomero, eneo la Kilombero-Rufiji, Tanzania

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Milima ya Udzungwa na Bonde la Kilombero.

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: 200 - 900 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Hyperolius rubrovermiculatus (Schjøtz, 1975)

Shimba Red-Vermiculated Reed Frog



E. Harper

SVL: ♂ 24 – 30 mm; ♀ 28 – 32 mm

DESCRIPTION: All individuals have light canthal and dorsolateral stripes and a light spot on each heel. In some individuals the dorsum is very dark with red spots while in others the dorsum is lighter with faint markings. The throat and ventral surfaces are yellow-orange and the feet are reddish.

SIMILAR SPECIES: *H. rubrovermiculatus* is possibly a subspecies of *H. mitchelli*. Their distributions do not overlap.

HABITAT: Coastal forests and formerly forested areas of Kenya

NATURAL HISTORY: See account for *H. mitchelli*

CALL: Schjøtz (1999) describes the call as “a series of brief screams”

DISTRIBUTION IN THE EACF: Known only from the Shimba Hills in Kenya

TYPE LOCALITY: Shimba Hills, Kenya

ELEVATIONAL RANGE: 140 – 350 m

CONSERVATION STATUS: Endangered

UREFU WA MWILI: ♂ 24 – 30 mm; ♀ 28 – 32 mm

MAELEZO: Vyura wote wana mistari iliyofifia kati ya pua na macho, mgongoni na pembeni na doa lililofifia kwenye kila wayo. Kwenye baadhi ya vyura, sehemu ya juu ni nyeusi sana na ina madoa mekundu; sehemu ya juu ya vyura wengine ina rangi na alama zilizofifia. Koo na sehemu ya chini ni njano-rangi ya machungwa na nyayo ni nyekundu nyekundu.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Inawezekana *H. rubrovermiculatus* ni spishi ndogo ya *H. mitchelli*. Spishi hizi mbili zinapatikana maeneo tofauti.

MAZINGIRA: Misitu ya Pwani na mahali palipokuwa na misitu awali.

HISTORIA ASILIA: Rejea taarifa za *H. mitchelli*.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Milima ya Shimba tu, Kenya.

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Milima vya Shimba, Kenya

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: 140 – 350 m

HALI YA UHIFADHI: Iko hatarini



Hyperolius spinigularis (Stevens, 1971)

Spiny-throated Reed Frog, Spiny Reed Frog, Mulanje Reed Frog



J. Vonesh

SVL: ♂ 24 < mm; ♀ < 28 mm

DESCRIPTION: A small *Hyperolius*. The dorsum is a translucent green or brown with pale canthal and dorsolateral stripes. In some individuals the entire area of the snout in front of the eyes may be white. Both males and females have small spines on the dorsum. In males the throat and undersides of the legs are covered with conspicuous black spines.

SIMILAR SPECIES: *H. spinigularis* is very similar in appearance to *H. tanneri*. The black spines on the throat of the males distinguish this species from others in the genus.

HABITAT: Wet areas of forest and agricultural land

NATURAL HISTORY: Clutches of unpigmented eggs are attached to vegetation over water. Females often return to egg masses on subsequent nights to deposit additional water, preventing the eggs from drying out. Tadpoles hatch and drop into the water after five days.

CALL: The call of *H. spinigularis* has not been recorded in the field; however captive individuals emit a quiet, high-pitched rasping call. It is unclear whether this is a territorial or mating call.

DISTRIBUTION IN THE EACF: Usambara, Uluguru, and Nguru Mountains and the Ruvu South Forest Reserve in the coastal lowlands of Tanzania

TYPE LOCALITY: Chisambo Tea Estate, Mulanje, Malawi

ELEVATIONAL RANGE: < 2000 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ 24 < mm; ♀ < 28 mm

MAELEZO: *Hyperolius* huyu ni mdogo. Sehemu ya juu ni kijani angavu au kahawia yenye mistari iliyofifia kati ya pua na macho, mgongoni na pembeni. Kwenye baadhi ya vyura, eneo lote la pua mbele ya jicho linaweza kuwa jeupe. Madume na majike yana miiba midogo sehemu ya juu. Kwenye madume, koo na sehemu ya chini ya miguu ina miiba mieusi inayojitokeza sana.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: *H. spinigularis* inafanana sana na *H. tanneri*. Mistari mieusi ya koo la madume inatofautisha spishi hii na zingine kwenye jenasi.

MAZINGIRA: Maeneo ya msituni yenye unyevu na ya kilimo.

HISTORIA ASILIA: Makundi ya mayai yasiyokuwa na rangi yanagandishwa kwenye uoto juu ya maji. Mara nyingi, majike yanarudi kwenye mayai usiku kuyawekea maji zaidi ili yasikauke. Viluwilwi vinatolewa na kuanguka majini baada ya siku tano.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMP: Milima ya Usambara, Uluguru, na Nguru na Hifadhi ya Mimitu ya Ruvu Kusini kwenye maeneo tambarare ya pwani, Tanzania

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Mulanje, Malawi

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: < 2000 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Hyperolius tanneri (Schjøtz, 1982)

Synonymous with *Hyperolius tannerorum* (Schjøtz, 1999)

Tanner's Reed Frog



E. Harper

SVL: ♂ 20 – 23 mm; ♀ 29 – 34 mm

DESCRIPTION: The dorsum is green with light canthal and dorsolateral stripes. Fingers and toes are yellow. The throat and ventral surface are blue-green.

SIMILAR SPECIES: *H. tanneri* is very similar in appearance to *H. spinigularis*, but *H. tanneri* lacks black spines on the throat and ventrum.

HABITAT: Undisturbed montane forest

NATURAL HISTORY: Breed in forest swamps. Eggs are unpigmented.

CALL: May not have an advertisement call.

DISTRIBUTION IN THE EACF: Known only from the type locality

TYPE LOCALITY: Mazumbai Forest Reserve, West Usambara Mountains, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: 1410 m

CONSERVATION STATUS: Endangered

UREFU WA MWILI: ♂ 20 – 23 mm; ♀ 29 – 34 mm

MAELEZO: Sehemu ya juu ni kijani yenye mistari iliyoifia kati ya pua na macho, mgongoni na pembeni. Vidole vya mikononi na miguuni ni njano. Koo na sehemu ya chini ni bluu kijani.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: *H. tanneri* inafanana sana na *H. spinigularis*, lakini haina mistari mieusi kwenye koo na sehemu ya chini.

MAZINGIRA: Misitu iliyopo zaidi ya 1200 m kutoka usawa wa bahari ambayo haijaguswa.

HISTORIA ASILIA: Inazaliana msituni kwenye vinamasi. Mayai hayana rangi.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Imepatikana tu mahali kielelezo kilipopewa jina kwa mara ya kwanza

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Hifadhi ya Misitu ya Mazumbai, Milima ya Usambara Magharibi, Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: 1410 m

HALI YA UHIFADHI: Iko hatarini



Hyperolius tuberlinguis (Smith, 1849)

Green Reed Frog, Tinker Reed Frog, Straw-or-green Sedge Frog,
Yellow-green Reed Frog, Smith's Reed Frog



R. Drewes

SVL: ♂ 25 – 33 mm; ♀ 30 – 40 mm

DESCRIPTION: A large *Hyperolius* with a broad head and a sharply pointed snout. Most individuals are solid yellow, tan or near translucent green, but some may be marked with a faint hourglass figure on the dorsum or a light triangle between the eyes. The throat is bright yellow in males and pale yellow in females. The insides of the legs are red.

SIMILAR SPECIES: Similar in appearance to *H. glandicolor* morphs that lack dorsal markings, but *H. tuberlinguis* has yellow rather than pink or red disks on the toes and fingers.

HABITAT: Abundant in coastal lowland savanna and grassland. Tolerates some degree of habitat modification and can be found in parks and agricultural areas.

NATURAL HISTORY: Males call from emergent vegetation around a wide variety of aquatic habitat types. Clutches of 240 – 400 unpigmented eggs are attached to vegetation over water. Tadpoles are brown with bright specks and the undersides are light in color. Tadpoles reach 45 mm in length. Mouthparts are small and not heavily keratinized.

CALL: Males call from vegetation near water. Schiøtz (1999) describes the call as “a series of slow, coarse creaks, sometimes two in rapid succession.”

DISTRIBUTION IN THE EACF: Throughout the Eastern Arc Mountains and coastal forests in Tanzania and Kenya.

TYPE LOCALITY: South Africa

ELEVATIONAL RANGE: < 1000 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ 25 – 33 mm; ♀ 30 – 40 mm

MAELEZO: *Hyperolius* huyu ni mkubwa na ana kichwa kipana na pua iliyochongoka sana. Vyura wengi ni njano au kijani angavu lakini baadhi yao wanaweza kuwa na umbo la “V” mbili zinazogusana moja ikiwa chini juu, kwenye sehemu ya juu au pembetatu iliyofifia kati ya macho. Koo la madume lina rangi ya njano angavu na kwa majike, njano iliyofifia. Sehemu ya ndani ya miguu ni nyekundu.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Inafanana na vyura wa *H. glandicolor* wakiwa kwenye hatua mbalimbali ambao hawana alama zozote sehemu ya juu. Lakini *Hyperolius tuberlinguis* ina ncha za vidole miguuni na mikononi zilizo njano na siyo rangi ya waridi

MAZINGIRA: Inapatikana kwa wingi kwenye maeneo ya savana na nyika tambarare ya pwani. Inavumilia mazingira yaliyobadilika kiasi na inapatikana kwenye hifadhi za taifa na maeneo ya kilimo.


HISTORIA ASILIA: Madume yanaita yakiwa kwenye uoto uliojitokeza juu ya maji kwenye mazingira ya aina nyingi ya maji. Makundi ya mayai 240 - 400 yasiyokuwa na rangi yanagandishwa kwenye uoto juu ya maji. Viluwiluwu ni kahawia na vina madoa madogo madogo yanayong'aa na sehemu ya chini yana rangi iliyofifia; vinafikia urefu wa 45 mm. Sehemu za mdomo ni ndogo na hazina umbile maalum kwa ajili ya kula

ENEO SPISHI INAPATIKANA KWENYE MTMMP: Maeneo yote ya MTMMP ya Tanzania na Kenya.

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Afrika ya Kusini

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: < 1000 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Kassina maculata (Duméril, 1853)

Vlei frog, Red-legged Kassina, Red-legged Pan frog, Spotted Running Frog



J. Vonesh

SVL: ♂ 55 mm; ♀ 65 mm

DESCRIPTION: A large, primarily aquatic frog with a gray dorsum covered in large dark spots outlined in white. The groin and inner parts of the thigh are bright red. The ventral surface is light often with dark mottling. Toe and finger tips are expanded into rounded disks. In females the area around the vent is covered with spines.

SIMILAR SPECIES: *K. maculata* is similar to *K. senegalensis*, but has distinctive bright red-orange markings on the thigh.

HABITAT: Common in savanna, grassland, and shrubland in coastal lowlands. Tolerates some degree of habitat alteration and may be found in agricultural areas.

NATURAL HISTORY: Breeding takes place in a wide range of temporary and permanent bodies of water. Egg masses are attached to submerged vegetation. Tadpoles reach 130 mm in length and have heavy beaks and high fins. The larval period can last as 10 months. The skin of *K. maculata* contains a variety of toxins to deter mammalian predators.

CALL: Males call while floating in the water, often propped on aquatic vegetation. The call is a single rising note repeated at irregular intervals.

DISTRIBUTION IN THE EACF: Coastal areas of Kenya and Tanzania

TYPE LOCALITY: Zanzibar Island, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: < 1400 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ 55 mm; ♀ 65 mm

MAELEZO: Chura huyu ni mkubwa sana na anaishi majini muda mwingi; sehemu ya juu ni kijivu yenye madoa makubwa meusi yaliyozungushiwa rangi nyeupe. Kinena na sehemu ya ndani ya mapaja ni nyekundu inayong'aa. Sehemu ya chini ina rangi iliyofifia na ina madoa meusi mara nyingi. Ncha za vidole vya miguuni na mikononi ni pana na mviringo. Kwenye majike, kuna miiba kwenye eneo linalozunguka tundu la kutolea haja na kutoa na kupokelea mbegu za uzazi.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: *K. maculata* inafanana na *K. senegalensis* lakini ina alama nyekundu njano inayong'aa kwenye mapaja

MAZINGIRA: Inapatikana kwa wingi kwenye savana, nyika na vichakani kwenye maeneo tambarare ya pwani. Inavumilia mazingira yaliyobadilika kiasi na inapatikana pia kwenye maeneo ya kilimo.


HISTORIA ASILIA : Inazaliana kwenye aina mbalimbali za maji ya kudumu au ya muda. Mayai yanagandishwa kwenye uoto ulio chini ya maji. Viluwilwi vinafikia urefu wa 130 mm na vina midomo mizito na pezi za juu. Mabadiliko hadi kufikia chura mchanga yanaweza kuchukua miezi 10. Ngozi ya *K. maculata* ina aina mbalimbali za sumu ili kujilinda dhidi ya mamalia wanaowawinda.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Pwani ya Kenya na Tanzania.

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Kisiwa cha Zanzibar, Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: < 1400 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Kassina senegalensis (Duméril and Bibron, 1841)

Senegal Running Frog, Running Frog, Senegal Land Frog,
Bubbling Kassina



R. Drewes

SVL: ♂ 33 – 40 mm; ♀ 33 – 40 mm

DESCRIPTION: The dorsum is pale gray with large dark spots and a broad, dark vertebral stripe. Toe and fingertips are expanded into small disks.

SIMILAR SPECIES: *K. senegalensis* lacks the bright red-orange markings that are present on the thigh of *K. maculata*. *K. senegalensis* may be composed of multiple cryptic species.

HABITAT: Found in a wide range of habitat types including savannas, shrubland, and grassland. Also tolerates degraded habitats.

NATURAL HISTORY: Breeding takes place in a range of temporary and aquatic habitat types, primarily pools with abundant vegetation. Clutches of 260 – 400 eggs are attached to submerged vegetation. Tadpoles are large with high tail fins.

CALL: Males call in groups of 3-10 from concealed positions in vegetation near, but not usually in, water. The call is a series of rising notes sounding like bubbles.

DISTRIBUTION IN THE EACF: Coastal and southern Kenya and throughout Tanzania

TYPE LOCALITY: Senegal

ELEVATIONAL RANGE: < 2000 m

UREFU WA MWILI: ♂ 33 – 40 mm; ♀ 33 – 40 mm

MAELEZO: Sehemu ya juu ni kijivu iliyofifia, ina madoa makubwa meusi na mstari mmoja mpana mgongoni.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: *K. senegalensis* haina alama nyekundu njano inayong'aa kama kwenye mapaja ya *K. maculate*. Inawezekana *K. senegalensis* inajumuisha spishi zingine ambazo bado hazjaainishwa.

MAZINGIRA: Inapatikana kwenye aina nyingi za mazingira pamoja na savana, vichaka na nyika. Inavumilia mazingira yaliyoharibiwa.


HISTORIA ASILIA; Inazaliana kwenye mazingira ya aina nyingi ya maji ya muda au ya kudumu, hususan kwenye madimbwi yenye uoto mwingi. Makundi ya mayai 260 - 400 yanagandishwa kwenye uoto uliopo chini ya maji. Viluwiluwi ni vikubwa na vina pezi zilizoinuka juu.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Pwani ya Kenya, Kusini mwa Kenya na mahali pote Tanzania

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Senegal

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: < 2000 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Phlyctimantis keithae (Schizøtz, 1975)

Keith's Striped Frog, Keith's Wot-wot



SVL: 39 – 43 mm

DESCRIPTION: The dorsum is black and covered with small white-tipped warts. Arms and legs are banded black and gray. The tympanum is small but distinctly visible. The ventral surface has blue and black mottling. Toes are expanded and end in small disks. Toes have a small amount of webbing. The base of the arms and the inner parts of the legs are bright red-orange and black.

SIMILAR SPECIES: Most similar to the *Kassina spp.* but easily distinguished by its white-tipped warts.

HABITAT: Found in forest, grassland and agricultural areas near forest.

NATURAL HISTORY: Forest dependent, but uses open areas for breeding. Males call from emergent vegetation around pools and ponds.

CALL: Channing and Howell (2006) describe the call as sounding like “wot-wot...pulsed....with a duration of 0.15 seconds...There are 8 pulses in a typical call.”

DISTRIBUTION IN THE EACF: Udzungwa Mountains

TYPE LOCALITY: Dabaga Forest, Udzungwa Mountains, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: 1800 – 2000 m

CONSERVATION STATUS: Vulnerable

UREFU WA MWILI: 39 – 43 mm

MAELEZO: Sehemu ya juu ni nyeusi na ina chunjua ndogo zenye ncha nyeupe. Mikono na miguu ina mistari mieusi na kijivu. Kiwambo cha sikio ni kidogo lakini kinaonekana. Sehemu ya chini ina madoa meusi. Vidole vya miguuni ni vipana na vina ncha mviringo na ndogo. Vidole vya miguuni vina utando kidogo. Mwanzo wa mikono na sehemu za ndani za miguu ni nyekundu machungwa ya kung'aa na nyeusi.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Inafanana sana na *Kassina spp* lakini ina chunjua zenye ncha nyeupe

MAZINGIRA: Inapatikana kwenye misitu, nyika na maeneo ya kilimo karibu na misitu.


HISTORIA ASILIA: Inapenda sana misitu lakini inazaliana kwenye maeneo wazi. Madume yanaita kutoka kwenye uoto uliojitokeza juu ya maji karibu na madimbwi.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Milima ya Udzungwa

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Misititu ya Dabaga, Milima ya Udzungwa, Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: 1800 – 2000 m

HALI YA UHIFADHI: Inaweza kuathiriwa



Microhylidae

Microhylids are geographically widespread, but several genera that occur in the Eastern Arc are found nowhere else in the world. *Parhoplophryne usambarica* is the only species in its genus and is known only from the East Usambara Mountains. *Hoplophryne rogersi* and *H. uluguruensis* are forest species that occur on only a few of the mountains in the Eastern Arc chain. *Spelaeophryne methneri* is a secretive burrowing frog endemic to Tanzania. *Phrynomantis bifasciatus*, in contrast, is a more widespread and disturbance tolerant species that is common throughout much of southern and central Africa. All five species of microhylids in the Eastern Arc are stout, burrowing frogs with short limbs and short snouts.

Microhylids zinapatikana maeneo mengi lakini spishi kadhaa zinazopatikana kwenye Tao la Mashariki hazipo mahali pengine popote duniani. *Parhoplophryne usambarica* ndiyo spishi pekee kwenye jenasi yake na inapatikana kwenye Milima ya Usambara Mashariki tu. Spishi za *Hoplophryne rogersi* na *H. uluguruensis* zinapatikana msituni na kwenye misitu michache tu ya milima ya Tao la Mashariki. Vyura wa spishi ya *Spelaeophryne methneri* wanajificha karibu wakati wote, wanachimba mashimo ardhini na wanapatikana Tanzania tu. Lakini spishi ya *Phrynomantis bifasciatus* inapatikana mahali pengi, inavumilia usumbufu na inapatikana sana karibu maeneo yote ya Afrika ya kati na kusini mwa Afrika. Spishi zote tano za microhylids zilizopo Tao la Mashariki ni nene, zinachimba mashimo ardhini, zina miguu na mikono mifupi na pua fupi.



Hoplophryne rogersi
J. Vonesh

Hoplophryne rogersi (Barbour and Loveridge, 1928)
Roger's Three-fingered Frog, Usambara Blue-bellied Frog



J. Vonesh

SVL: ♂ & ♀ 23 – 28 mm

DESCRIPTION: A small frog with a smooth dorsum that is dark gray with darker blotches. The short snout comes to a sharp point. A dark band extends from the tip of the snout, under the eye to the base of the arm. The ventral surface is dark with small white blotches. The tips of the fingers and toes are slightly expanded and truncated. Females have only three fingers, while in males the first finger (or 'thumb') is modified into a spiny projection that presumably aids in clasping the female during mating. Males in breeding condition have enlarged glands in the pectoral region and on the arms.

SIMILAR SPECIES: There are no known similar species within the geographic range of *H. rogersi*.

HABITAT: Lowland and montane forest

NATURAL HISTORY: Typically found only during the breeding season. Breeding takes place in water-filled tree holes or bamboo cups. A small number of unpigmented eggs are laid

on the vertical surface above the water. The pale tadpoles are slender with long tails. They possess a unique structure on the abdomen, a 'belly-finger,' which allows them to maneuver in small spaces.

CALL: Unknown

DISTRIBUTION IN THE EACF: Usambara, Magrotto and Nguru Mountains

TYPE LOCALITY: Mt. Bomoli, Amani, East Usambara Mountains, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: 600 – 1200 m

CONSERVATION STATUS: Endangered

UREFU WA MWILI: ♂ & ♀ 23 – 28 mm

MAELEZO: Chura huyu ni mdogo na sehemu ya juu ni laini, kijivu iliyokolea na madoa yaliyokolea zaidi. Pua yake fupi ina ncha iliyochongoka. Kuna mstari mweusi kutoka ncha ya pua chini ya jicho hadi mwanzo wa mkono. Sehemu ya chini ni nyeusi na ina madoa madogo meupe. Ncha za vidole vya mkononi na miguuni ni pana kidogo na butu. Majike yana vidole vya mkononi vitatu tu; kidole cha tatu (kidole gumba) cha mkononi cha madume ni kama mwiba unaojichomoza, ambao unalisaidia dume kulikamata jike wakati wa kupandana. Wakati wa msimu wa kupandana, madume yanakuwa na tezi pana kifuani na mikononi.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Hakuna spishi zinazofanana nayo zinazojulikana kwenye maeneo inapokatikana.

MAZINGIRA: Misitu ya maeneo tambarare na zaidi ya 1200 m kutoka usawa wa bahari.

HISTORIA ASILIA: Inapatikana wakati wa msimu wa kuzaliana. Inazaliana kwenye mashimo ya miti yaliyojaa maji au mashimo ya kwenye mashina ya mianzi. Idadi ndogo ya mayai yasiyokuwa na rangi yanatagwa kwenye upande ulio wima juu ya maji. Viluwiluwi wana rangi iliyofifia, ni wembamba na wana mikia mirefu. Wana umbo la pekee kwenye tumbo linalowawezesha kupita penye nafasi ndogo.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Milima ya Usambara, Magrotto na Nguru

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Mlima Bomoli, Amani, Milima ya Usambara Mashariki, Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI:
600 – 1200 m

HALI YA UHIFADHI: Ipo hatarini



Hoplophryne uluguruensis (Barbour & Loveridge, 1928)
Uluguru Three-fingered Frog, Uluguru Blue-bellied Frog



SVL: ♂ < 25 mm; ♀ < 21 mm

DESCRIPTION: A robust, flat frog with a small head. The dorsum is uniform dark brown to black and smooth. A fold of skin angles from the eye to the base of the arm. The first finger is reduced and in males has three spines. Toe tips are expanded. Toes lack webbing. The ventral surface is yellow-brown without markings. Males have short, fat arms and legs with light-colored spines on the legs.

SIMILAR SPECIES: This species is similar to *Hoplophryne rogersi*, but their distributions do not overlap.

HABITAT: Undisturbed montane forest

NATURAL HISTORY: Eggs are laid in water-filled tree holes, leaf axils, banana leaves or bamboo.

CALL: Unknown

DISTRIBUTION IN THE EACF: Uluguru and Udzungwa Mountains

TYPE LOCALITY: Mt. Mbova above Nyange, Uluguru Mountains, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: Unclear, but can be found above 1200 m

CONSERVATION STATUS: Vulnerable

UREFU WA MWILI: ♂ < 25 mm; ♀ < 21 mm

MAELEZO: Chura huyu ana nguvu, ni bapa na ana kichwa kidogo. Sehemu ya juu ni kahawia iliyokolea hadi nyeusi na laini. Kunjo la ngozi linatoka jichoni hadi mwanzoni mwa mkono. Kidole cha kwanza cha mkononi kimeingia ndani na kina miiba mitatu kwenye madume. Ncha za vidole vya mguuni ni vipana. Vidole vya mguuni havina utando. Sehemu ya chini ni njano kahawia na hakuna alama zozote. Madume yana miguu na mikono mifupi, minene na kuna miiba yenye rangi iliyofifia kwenye miguu.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Spishi hii inafanana na *Hoplophryne rogersi* lakini maeneo zinapokatikana spishi hizi mbili ni tofauti.

MAZINGIRA: Mimitu zaidi ya 1200 kutoka usawa wa bahari ambayo haijaguswa

HISTORIA ASILIA: Mayai yanatagwa kwenye mashimo ya miti yaliyojaa maji, kwenye sehemu iliyo kati ya kikonyo na shina la majani, majani ya ndizi au mianzi.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Milima ya Uluguru na Udzungwa

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Mlima Mbova, Milima ya Uluguru, Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: > 1200 m

HALI YA UHIFADHI: Inaweza kuathiriwa.



Parhoplophryne usambarica (Barbour & Loveridge, 1928)

Amani Forest Frog, Usambara Black-banded Frog



This species has not been seen since the 1920's and may be extinct

SVL: ♀ < 23 mm

DESCRIPTION: A small stout frog. The dorsum is gray-blue with a black stripe that runs from the snout to the eye, along the side and upper leg ending at the knee. The ventral surface is black with blue and white vermiculations. Toes lack webbing and toe tips are not expanded. The legs are barred. Males have blue glands on the arms and chest.

SIMILAR SPECIES: Similar to the *Hoplophryne* species, but in *Hoplophryne* the first finger is reduced and spines are present in males.

HABITAT: Leaf litter in submontane forest

NATURAL HISTORY: Unknown

CALL: Unknown

DISTRIBUTION IN THE EACF: Known only from the type locality

TYPE LOCALITY: West of Amani, Usambara Mountains, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: 900 m

CONSERVATION STATUS: Critically endangered

Spishi hii haijaonekana tangu miaka ya 1920 na huenda imetoweka.

UREFU WA MWILI: ♀ < 23 mm

MAELEZO: Chura huyu ni mdogo na mnene. Sehemu ya juu ni kijivu bluu na kuna mstari mweusi kutoka puani hadi kwenye jicho, pembeni mwa mwili na kwenye sehemu ya juu ya mguu na kuishia kwenye goti. Sehemu ya chini ni nyeusi na ina mistari bluu na mieupe iliyopindapinda. Vidole vya miguuni havina utando na ncha za vidole hivyo siyo pana. Miguu ina mistari. Madume yana tezi za bluu mkononi na kifua.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Inafanana na *Hoplophryne* lakini kidole cha kwanza cha mikononi cha *Hoplophryne* ni butu na madume yake yana miiba.

MAZINGIRA: Msituni kwenye majani yalioanguka chini, kwenye maeneo yaliyopo takribani 1200 m kutoka usawa wa bahari

HISTORIA ASILIA: Haijulikani

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Mahali ambapo kielelezo kilipewa jina kwa mara ya kwanza

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Magharibi mwa Amani, Milima ya Usambara, Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: 900 m

HALI YA UHIFADHI: Iko hatarini sana



Phrynomantis bifasciatus (Smith, 1847)

Two-striped Frog, Red-banded Frog, Banded Rubber Frog



R. Drewes

SVL: ♂ < 53 mm; ♀ < 65 mm

DESCRIPTION: A large shiny black frog with two bright red-orange stripes running from the eyes to the groin. There is also a large red spot above the vent. The arms and legs are covered in red spots. The tympanum is visible in red spots. The tympanum is slightly smaller than the eye. Toe and finger tips are expanded and end in small truncate disks. The ventral surface is gray with white spots.

SIMILAR SPECIES: The coloration of this species is distinctive.

HABITAT: Grasslands and wooded

savanna. Tolerates some habitat modification and can be found in agricultural areas

NATURAL HISTORY: Breeding takes place in flooded grasslands and temporary pools during the summer rainy season. Clutches are deposited directly in water and contain 300 – 1500 eggs.

CALL: Channing and Howell (2006) describe the call as “a long melodious trill, lasting up to 3 seconds.”

DISTRIBUTION IN THE EACF: Throughout the Eastern Arc and Coastal Forests in Tanzania and Kenya

TYPE LOCALITY: Limpopo Province, South Africa

ELEVATIONAL RANGE: 50 – 1450 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ < 53 mm; ♀ < 65 mm

MAELEZO: Chura huyu ni mkubwa anayeng'aa na ana mistari miwili njano inayong'aa kutoka machoni hadi kwenye kinena. Aidha, kuna doa moja kubwa jekundu juu ya tundu la kutolea haja na kutoa na kupokelea mbegu za uzazi. Mikono na miguu ina madoa mekundu. Kiwambo cha sikio kinaonekana na kidogo kiasi kuliko jicho. Ncha za vidole vya mguuni na mkononi ni pana na mviringo. Sehemu ya chini ni kijivu na ina madoa meupe.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Rangi ya spishi hii inamtofautisha na spishi zingine

MAZINGIRA: Nyika na savana yenye miti. Inavumilia mazingira yaliyoharibiwa kiasi na inapatikana kwenye maeneo ya kilimo.


HISTORIA ASILIA: Inazaliana kwenye nyasi zilizofurika maji na madimbwi ya muda wakati wa msimu wa mvua na joto. Makundi yanakuwa na mayai 300 – 1,500 yanayotagwa moja kwa moja kwenye maji.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Maeneo yote ya MTMMP ya Tanzania na Kenya.

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Jimbo la Limpopo, Afrika ya Kusini

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: 50 – 1450 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Spelaeophryne methneri (Ahl, 1924)

African Striped Frog, Scarlet-snouted Frog



SVL: < 53 mm

DESCRIPTION: The dorsum is black with bright red canthal stripes that extend over the eye to above the tympanum. There is a fold of skin running from the eye to the arm. There is some variation among individuals, with some having a red stripe between the eyes and others lacking any red markings on the head. The tympanum is visible and approximately the same size as the eye. The finger and toe tips are not expanded. The ventral surface is brown.

SIMILAR SPECIES: This is the only species in its genus

HABITAT: Moist lowland and montane forest, savanna, and miombo woodland

NATURAL HISTORY: A secretive species that burrows into rotting logs. Breeding habits are unknown, but it is assumed to lay eggs that hatch directly into small frogs.

CALL: Unknown

DISTRIBUTION IN THE EACF: Uluguru and Udzungwa Mountains and Mt. Rungwe

TYPE LOCALITY: Nangoma Cave, Matumbi near Kilwa, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: < 1600 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: < 53 mm

MAELEZO: Sehemu ya juu ni nyeusi; ina mistari miekundu inayong'aa kati ya pua na macho, inayotoka juu ya jicho hadi juu ya kiwambo cha sikio. Kuna mkunjo wa ngozi kutoka jichoni hadi mkononi. Kuna tofauti baina ya vyura, baadhi wana mstari mwekundu kati ya macho na wengine hawana alama nyekundu yoyote kichwani. Kiwambo cha sikio kinaonekana na ukubwa wake ni takribani sawa na wa jicho. Vidole vya mkononi na mguuni siyo vipana. Sehemu ya chini ni kahawia.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Ni spishi peke yake kwenye jenasi

MAZINGIRA: Maeneo tambarare yenye maji na misitu iliyopo zaidi ya 1200 m kutoka usawa wa bahari, savana na miombo

HISTORIA ASILIA: Spishi hii inajificha kwenye magogo yanayooza. Mfumo wa uzalishaji haujulikani lakini inadhaniwa kwamba inataga mayai na viluwiluwi vinatolewa moja kwa moja


ENEO INAPOPATIKANA SPISHI KWENYE MILIMA YA TAO LA MASHARIKI NA

MISITU YA PWANI: Milima ya Uluguru, Udzungwa na Rungwe

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Pango ya Nangoma, Matumbi, Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: < 1600 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Petropedetidae

The family Petropedetidae is confined to sub-Saharan Africa. Two species, both in the genus *Petropedetes*, can be found in the Eastern Arc Mountains. They are typically found in or near rocky streams. Both species have toe and finger disks that are distinctly divided into two lobes.

Familia ya Petropedetidae inapatikana Afrika kusini mwa Sahara tu. Spishi mbili, zote zikiwa kwenye jenasi ya *Petropedetes*, zinapatikana Milima ya Tao la Mashariki. Kwa kawaida, chura hawa wanaishi karibu na au kwenye vijito vyenye miamba. Spishi zote mbili zina ncha butu za vidole vya miguuni na mikononi zilizogawanyika katika ndewe.



Petropedetes eggs.

J. Vonesh



Petropedetes yakusini
E. Harper

Petropedetes martiensseni (Nieden, 1911)

Tanzania Rocky River Frog, Usambara Montane Torrent Frog,
Martienssen's Torrent Frog, Usambara Torrent Frog



J. Vonesh

SVL: ♂ 74 mm; ♀ 50 – 67 mm

DESCRIPTION: A large frog usually found near rocky streams. The dorsum is light tan or brown with irregular darker blotches, and usually with a rosy tinge to the limbs. The dorsal surface is granular in texture with a few scattered bumps and ridges. A fold of skin stretches from the eye to the base of the arm over the tympanum. The tympanum is visible and is smaller than the eye. Toe and finger tips are expanded into heart-shaped disks. Fingers lack webbing, and toes are webbed only

slightly at the base. Males in breeding condition have thick arms.

SIMILAR SPECIES: *Petropedetes yakusini* is similar in appearance, but the ranges of the two species do not overlap.

HABITAT: Rocky forest streams in undisturbed forest

NATURAL HISTORY: Eggs are laid on wet rocks near streams or seepage areas. Tadpoles have wide mouths that allow them to cling to and graze on the surface of rocks. Metamorphs are around 12 mm in length. Outside of the breeding season adults are found on the forest floor in holes and among rocks.

CALL: Males call from rocky crevices near running water. The call is a loud, deep single note.

DISTRIBUTION IN THE EACF: East and West Usambara Mountains

TYPE LOCALITY: Tanga, Usambara Mountains, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: 600 – 1800 m

CONSERVATION STATUS: Endangered

UREFU WA MWILI: ♂ 74 mm; ♀ 50 – 67 mm

MAELEZO: Chura huyu ni mkubwa sana na anapatikana kwenye vijito vyenye miamba. Sehemu ya juu ni hudhuru iliyoifia au kahawia na ina madoa meusi yasiyokuwa na mpangilio, na mara nyingi kunakuwa na rangi ya waridi kwenye mikono na miguu. Sehemu ya juu ina chembechembe, nundu na matuta machache. Mkunjo wa ngozi unatoka jichoni hadi kiwambo cha sikio na mwanzoni mwa mkono. Kiwambo cha sikio kinaonekana na ni kidogo kuliko jicho. Ncha za vidole vya mguuni na mkononi ni pana na zina umbo la moyo. Vidole vya mkononi havina utando na vidole vya mguuni vina utando kidogo mwanzoni. Madume yanakuwa na mikono minene yakiwa kwenye msimu wa kupandana.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Inafanana na *Petropedetes yakusini* lakini spishi hizi mbili hazipatikani mahali pamoja.

MAZINGIRA: Vijito vya misituni vyenye miamba kwenye misitu ambayo haijaguswa


HISTORIA ASILIA: Mayai yanatagwa kwenye miamba yenye unyevu karibu na vijito au maeneo maji yanapovuja. Viluwiluwi vina midomo mipana inayoviwzesha kujishikilia na kula kwenye miamba. Urefu wa vyura wachanga ni 12 mm. Nje ya msimu wa kuzaliana, vyura wazima wanapatikana kwenye mashimo ardhini kwenye msitu au miamba.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Milima ya Usambara Magharibi na Usambara Mashariki

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Tanga, Milima ya Usambara, Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: 600 – 1800 m

HALI YA UHIFADHI: Iko hatarini



Petropedetes yakusini (Channing, Moyer, and Howell, 2002)
Southern Torrent Frog



E. Harper

SVL: ♂ < 73 mm; ♀ 68 mm

DESCRIPTION: A large frog with a broad head. The dorsum is gray to brown with dark markings. The tympanum is visible and slightly smaller than $\frac{1}{2}$ the diameter of the eye. Toe tips are expanded with bifurcate disks. Toes have a small amount of webbing. The throat and the back of the thighs are dark with small white speckling. The ventral surface is lighter than the dorsum and has lighter speckling. Males in breeding condition have a round, dark black protuberance on the upper part of the tympanum.

SIMILAR SPECIES: Similar to *Petropedetes martiensseni*, but their ranges do not overlap.

HABITAT: Rocky streams in undisturbed montane forest

NATURAL HISTORY: Breeding peaks during the short rains in November. Eggs are laid on wet rocks near streams or seepage areas. Tadpoles have wide mouths that allow them to cling to and graze on the surface of rocks. Outside of the breeding season adults are found on the forest floor in holes and among rocks near streams.

CALL: Channing and Howell (2006) describe the call as “a series of short ‘wauks’ repeated at long intervals of up to 25 seconds.”

DISTRIBUTION IN THE EACF: Uluguru, Udzungwa and Mahenge Mountains, Tanzania

TYPE LOCALITY: Njokomoni River, Udzungwa Mountains National Park, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: 300 – 1950 m

CONSERVATION STATUS: Endangered

UREFU WA MWILI: ♂ < 73 mm; ♀ 68 mm

MAELEZO: Chura huyu ni mkubwa sana na ana kichwa kipana. Sehemu ya juu ni kijivu hadi kahawia na kuna alama nyeusi. Kiwanbo cha sikio kinaonekana na ni chini ya $\frac{1}{2}$ ya kipenyo cha jicho. Ncha za vidole vya miguuni ni pana, mvingiro na zinagawanyika. Vidole vya mguuni vina utando kidogo. Koo na sehemu ya nyuma ya mapaja ni nyeusi na ina madoa madogo meupe meupe. Sehemu ya chini ina rangi iliyofifia zaidi kuliko sehemu ya juu na ina madoa yaliyofifia. Madume yaliyo kwenye msimu wa kupandana yana sehemu mvingiro na nyeusi inayojitokeza kwenye sehemu ya juu ya kiwanbo cha sikio.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Inafanana na *Petropedetes martiensseni* lakini spishi hizi hazipatikani mahali pamoja.

MAZINGIRA: Vijito vyenye miamba kwenye misitu isiyoguswa iliyopo zaidi ya 1200 m kutoka usawa wa bahari.

HISTORIA ASILIA: Kuzaliana kunafikia kilele wakati wa mvua za vuli mwezi Novemba. Mayai yanatagwa kwenye miamba yenye unyevu karibu na vijito au maeneo maji yanapovuja. Viluwilwi vina midomo mipana inayoviwezesha kujishikilia na kula kwenye miamba. Inapokuwa siyo msimu wa kuzaliana, vyura wazima wanapatikana kwenye mashimo ardhini kwenye msitu au miamba.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Milima ya Uluguru, Udzungwa na Mahenge, Tanzania

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Mto Njokomoni, Hifadhi ya taifa ya Milima ya Udzungwa, Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: 300 – 1950 m

HALI YA UHIFADHI: Iko hatarini



Phrynobatrachidae

The “puddle frogs” are small brown frogs with variable color patterns and small raised bumps on the dorsum. They are commonly found near puddles, streams or flooded grassy areas. Several new species have been discovered recently and there are likely many undescribed species. The family is confined to sub-Saharan Africa.

“Vyura wa vidimbwi” hawa ni wadogo na kahawia wenye mipangilio ya rangi inayotofautiana na wana nundu ndogo zilizo inuka kwenye sehemu ya juu. Chura hawa hupatikana karibu na vidimbwi, vijito au maeneo ya mafuriko yenye majani. Hivi karibuni, spishi kadhaa mpya ziligunduliwa na inaelekea kuna spishi nyingi ambazo bado hazina maelezo ya sifa zao. Familia hii inapatikana tu Afrika kusini mwa Sahara.



Phrynobatrachus
E. Harper

Phrynobatrachus acridoides (Cope, 1867)

East African Puddle Frog, Zanzibar Puddle Frog, Cope's Toad-frog, Eastern Puddle Frog



E. Harper

SVL: ♂ 28 mm; ♀ 30 mm

DESCRIPTION: A small gray-brown frog. The dorsal pattern is variable, often with a green or tan middorsal stripe or band and/or stripes on the legs. The dorsum is bumpy in most individuals, often with paired chevron shaped ridges between the arms. A fold of skin arches from the eye to the arm over the clearly visible tympanum. The tympanum is smaller than the eye. Toe and finger tips are faintly expanded, but lack distinct disks. Toes are partially webbed, but the extent of webbing varies somewhat

among individuals. The ventral surface is smooth and pale, usually with a yellowish tinge near the vent. In males the throat is uniform light gray or black. Females have mottled throats.

SIMILAR SPECIES: Larger than *P. ukingensis*. Can be distinguished from other species in the genus by the black or gray throat of the males, expanded finger tips and visible tympanum.

HABITAT: Forest, grassland, shrubland and savannas. Tolerates a degree of habitat alteration.

NATURAL HISTORY: Breeding takes place in still water including ponds, pools, swamps and ditches. Small dark eggs are laid in a single layer that floats just below the surface of the water or is attached to grass.

CALL: Males call while propped on vegetation in shallow water. The call is a continual harsh creaking snore, also described as "cricket-like"

DISTRIBUTION IN THE EACF: Eastern Tanzania

TYPE LOCALITY: Zanzibar Island, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: Usually below 700 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ 28 mm; ♀ 30 mm

MAELEZO: Chura huyu ni mdogo na kijivu kahawia. Mpangilio wa sehemu ya juu unatofautiana na mara nyingi kuna mstari wa kijani au hudhurungi katikati ya sehemu ya juu au mistari kwenye miguu. Sehemu ya juu ina nundu kwenye vyura wengi na mara nyingi kuna matuta mawili mawili yenye umbo la "V" kati ya mikono. Mkunjo wa ngozi unatoka kwenye jicho, unapita juu ya kiwambo cha sikio kinachoonekana hadi mkononi. Kiwambo cha sikio ni kidogo kuliko jicho. Vidole vya mguuni na mkononi vipana kidogo lakini havina ncha mwingiro zinazoonekana. Vidole vya miguuni vina utando kiasi lakini kuenea kwa utando kunatofautiana baina ya vyura. Sehemu ya chini ni laini, imefia na mara nyingi ni njano njano karibu na tundu la kutolea haja na kutoa na kupokelea mbegu za uzazi. Koo la madume ni kijivu iliyofifia au jeusi. Majike yana koo lenye madoa.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Spishi hii ni kubwa kuliko *P. ukingensis* Koo jeusi au kijivu la madume, ncha pana za vidole vya mkononi na kiwambo cha sikio vinaitofautisha spishi hii na zingine kwenye jenasi.

MAZINGIRA: Misit, nyika, vichaka na savana. Inavumilia mazingira yaliyobadilika kiasi.

HISTORIA ASILIA: Inazaliana kwenye maji yaliyosimama ya madimbwi, vinamasi na mifereji. Mayai madogo na meusi yanatagwa kwenye tabaka moja linaloelea chini kidogo ya maji au linagandishwa kwenye majani.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Kaskazini Tanzania

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA

MARA YA KWANZA: Kisiwa cha Zanzibar, Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI:
< 700 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini.



Phrynobatrachus kreffti (Boulenger, 1909)
Kreff's River Frog, Krefft's Puddle Frog



E. Harper

SVL: ♂ 36 mm; ♀ 41mm

DESCRIPTION: The dorsum is pale yellowish brown to dark reddish brown, sometimes with broad pale dorsolateral stripes or a pale triangle on the snout. Most individuals have a light tan stripe between the eyes. Toe and finger tips are distinctly swollen. Toes are approximately ½ webbed. The tympanum is visible, but is small and not particularly distinct. Females have pale throats. In males the throat is bright yellow, thumb pads are present and there are sharp spines on the toes.

SIMILAR SPECIES: The bright yellow throat of *P. kreffti* males is distinctive. *P. scheffleri* males also have yellow on the throat, but not as bright. Also, *P. scheffleri* do not have a visible tympanum.

HABITAT: Montane and submontane forest. Tolerates a moderate degree of habitat alteration, but is always found near forest.

NATURAL HISTORY: Males are territorial, and have been observed to approach one another and inflate their large, bright yellow vocal sacs without emitting any sound. This is presumably a territorial display. Males call during the day in shallow water, usually in rocky areas with vegetation. Egg masses, containing around 15 – 30 darkly pigmented eggs, are attached to rocks or vegetation near the water. Tadpoles are brown with two golden spots on the head.

DISTRIBUTION IN THE EACF: East and West Usambara Mountains and Magrotto Mountains

TYPE LOCALITY: Amani, East Usambaras, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: 700 – 1500 m

CONSERVATION STATUS: Endangered

UREFU WA MWILI: ♂ 36 mm; ♀ 41mm

MAELEZO: Sehemu ya juu ni njano iliyoifia kahawia hadi nyekundu kahawia, na wakati mwingine kuna mistari mipana mgongoni na pembeni au pembetatu iliyoifia kwenye pua. Idadi kubwa ya vyura ina mstari hudhurungi uliyoifia kati ya macho. Vidole vya miguuni na mkononi vimevimba sana. Vidole vya miguuni vina utando kwa ½. Kiwambo cha sikio kinaonekana lakini ni kidogo na hakijitokezi sana. Majike yana koo lenye rangi iliyoifia. Madume yana koo la njano inayong'aa, kuna uvimbe kwenye ngozi chini ya kidole gumba na miiba iliyoichongoka kwenye vidole vya miguuni.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Madume ya *P. kreffti* yana koo la njano inayong'aa. Aidha, madume ya *P. scheffleri* yanaweza pia kuwa na koo la njano lakini lisilong'aa. *P. scheffleri* hana kiwambo cha sikio kinachoonekana.

MAZINGIRA: Misitu iliyopo karibu au zaidi ya 1200 m kutoka usawa wa bahari. Inavumilia mabadiliko kiasi ya mazingira lakini inapatikana karibu na misitu wakati wote.


HISTORIA ASILIA: Madume yanalinda maeneo yao na yameonekana yakisogelea wenzao na kutunisha vifuko vyao vya sauti vikubwa na njano inayong'aa bila kutoa mlio wowote. Inadhaniwa kuwa hii ni njia ya kulinda eneo lao. Madume yanaita yakiwa kwenye maji yenye kina kifupi, kwenye uoto na miamba. Makundi yenye mayai 15 - 30 yenye rangi nyeusi yanagandishwa kwenye miamba au uoto karibu na maji. Viluwiluwi ni kahawia na vina madoa mawili kichwani yenye rangi ya dhahabu.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Milima ya Usambara Magharibi, Usambara Mashariki na Magrotto

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Amani, Usambara Mashariki, Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: 700 – 1500 m

HALI YA UHIFADHI: Iko hatarini



Phrynobatrachus natalensis (Smith, 1849)
Snoring Puddle Frog, Natal Dwarf Puddle Frog



M. Menegon

SVL: ♂ 34 mm; ♀ 40 mm

DESCRIPTION: Most individuals are dark brown with variable dorsal patterns including light vertebral stripes and bands. Finger tips lack disks or distinct swelling. The tympanum is visible and larger than ½ the diameter of the eye. Webbing is not consistent, possibly because of taxonomic confusion.

SIMILAR SPECIES: This species is likely a complex of multiple cryptic species. It can be distinguished from other *Phrynobatrachus* species in the EACF by its visible tympanum and lack

of expanded finger and toe tips.

HABITAT: Vegetation on the edges of water in forest, grassland, savanna and agricultural areas.

NATURAL HISTORY: Breeds in a wide range of aquatic habitat types, usually in still water including temporary pools and streams. Small dark brown eggs are laid in clutches of approximately 200. Metamorphosis is typically completed within 40 days.

CALL: Males can be heard calling during the day as well as at night. Channing and Howell (2006) describe the call as “a slow quiet snore”

DISTRIBUTION IN THE EACF: Eastern Tanzania

TYPE LOCALITY: Durban, South Africa

ELEVATIONAL RANGE: < 2200 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ 34 mm; ♀ 40 mm

MAELEZO: Idadi kubwa ya vyura ni kahawia iliyokolea na wana mipangilio mbalimbali sehemu ya juu, ikiwa ni pamoja na mistari yenye rangi iliyofifia kwenye mgongo. Vidole vya mkononi havina ncha mvingo au uvimbe unaoweza kuona. Kiwambo cha sikio kinaonekana na kinazidi ½ ya kipenyo cha jicho. Utando unatofautiana, labda kutokana na utata uliopo katika kuainisha spishi mbalimbali.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Inawezekana spishi hii inajumuisha spishi zingine ambazo hazijaainishwa bado. Tofauti na spishi zingine za MTMP, spishi hii ina kiwambo cha sikio kinachoonekana na haina ncha pana za vidole vya mguuni wala mkononi.

MAZINGIRA: Msituni kwenye uoto kando kando ya maji, nyika, savana na maeneo ya kilimo.


HISTORIA ASILIA: Inazaliana kwenye aina nyingi za mazingira ya maji, kwa kawaida kwenye maji yaliyosimama, pamoja na madimbwi ya muda na vijito. Mayai madogo na kahawia yanatagwa kwenye makundi yenye takribani mayai 200. Mabadiliko yote yanatokea ndani ya siku 40.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMP: Kaskazini Tanzania

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Durban, Afrika ya Kusini

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: < 2200 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Phrynobatrachus rungwensis (Loveridge, 1932)

Rungwe River Frog, Rungwe Puddle Frog



SVL: < 24 mm

DESCRIPTION: A small brown frog with darker markings on the dorsum and raised bumps. The tympanum is not visible. Males have mottled gray throats. Finger tips are slightly swollen, but lack distinct disks. Toes have small disks and are only partially webbed. The legs are barred.

SIMILAR SPECIES: Similar to *P. scheffleri*, and *P. uzunguensis* but the throat of males is gray in *P. rungwensis*. *P. rungwensis* can be distinguished from other species in the genus by its lack of a visible tympanum, its slightly swollen finger tips and disks on the toes.

HABITAT: Grassy pools and puddles in miombo woodland, savannas and montane grassland.

NATURAL HISTORY: The natural history of this species is not well known.

CALL: Unknown

DISTRIBUTION IN THE EACF: Udzungwa Mountains

TYPE LOCALITY: Ilolo, Rungwe Mountain, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: 1000 – 2000 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: < 24 mm

MAELEZO: Chura huyu ni mdogo, kahawia na ana alama zenye rangi iliyokolea zaidi na nundu zilizochochoza kwenye sehemu ya juu. Kiwambo cha sikio hakionekani. Madume yana madoa kijivu kwenye koo. Vidole vya mkononi vimevimba lakini havina ncha mviringo zinazoonekana. Vidole vya mguuni vina ncha ndogo mviringo na utando kiasi. Miguu ina mistari.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Inafanana na *P. scheffleri* na *P. uzunguensis* lakini koo la madume ya *P. rungwensis* ni kijivu. Aidha, *P. rungwensis* ni tofauti na spishi zingine za jenasi kwani haina kiwambo cha sikio kinachoonekana, ina ncha za vidole vya mkononi vilivyovimba kidogo na ncha mviringo kwenye vidole vya mguuni.

MAZINGIRA: Madimbwi yenye nyasi kwenye miombo, savana na nyika zilizopo zaidi ya 1200 m kutoka usawa wa bahari.


HISTORIA ASILIA: Haijulikani vizuri

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Milima ya Udzungwa

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Ilolo, Mlima Rungwe, Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: 1000 – 2000 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Phrynobatrachus scheffleri (Nieden, 1911)

Scheffler's Puddle Frog



E. Harper

SVL: ♂ 16 - 20 mm; ♀ 18 - 22 mm

DESCRIPTION: A small brown frog with raised bumps on the dorsum between the arms. A dark triangle between the eyes points toward the rear. The males have yellow throats and females have white throats. The tympanum is not visible. Toes have only slight webbing. Finger and toe tips are slightly expanded, but lack distinct disks.

SIMILAR SPECIES: Taxonomists previously confused *P. scheffleri* with *P. minutus*. The taxonomy is still not well defined. Both *P. scheffleri* and *P. krefftii*

males have yellow on their throats, but in *P. krefftii* the tympanum is visible.

HABITAT: Leaf litter, frequently found in dry shady stream beds, often clustered around small stony pools.

NATURAL HISTORY: Males call from vegetation near water. Eggs are laid during both rainy seasons and float in a raft on the water.

DISTRIBUTION IN THE EACF: Throughout the Eastern Arc Mountains and Coastal Forest of Kenya and Tanzania, also on the island of Zanzibar

TYPE LOCALITIES: Kibwesa, Mpapua and Zanzibar, Tanzania; Nairobi, Kenya

ELEVATIONAL RANGE: 0 – 1800 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ 16 - 20 mm; ♀ 18 - 22 mm

MAELEZO: Chura huyu ni mdogo na ana nundu zilizochomoza kwenye sehemu ya juu, kati ya mikono. Kuna pambetatu nyeusi kati ya macho na inayotazama nyuma. Madume yana koo njano na majike, koo jeupe. Kiwambo cha sikio hakionekani. Vidole vya mguuni vina utando kidogo sana. Vidole vya mkononi na mguuni ni vipana kidogo lakini havina ncha mviringo.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: *P. minutus* na *P. krefftii*

MAZINGIRA: Majani yaliyoanguka chini, wakati mwingi kwenye vijito vilivyokauka na vyenye kivuli na mara nyingi vyura wanajikusanya eneo linalozunguka madimbwi madogo yenye mawe.

HISTORIA ASILIA: Madume yanaita kutoka kwenye uoto karibu na maji. Mayai yanatagwa wakati wa misimu miwili ya mvua na yanaelea kwenye chelezo juu ya maji.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Maeneo yote ya Tanzania na Kenya, na kisiwa cha Zanzibar

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Kibwesa, Mpapua na Zanzibar, Tanzania na Nairobi, Kenya

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: 0 – 1800 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Phrynobatrachus ukingensis (Loveridge, 1932)

Ukinga River Frog, Ukinga Puddle Frog



SVL: ♂ 19 mm; ♀ 21 mm

DESCRIPTION: Very small frogs with smooth brown skin and flat bumps. Some individuals have light vertebral lines or bands on the dorsum and/or lines on the legs. Males have black throats. Toes end in distinct disks. The tips of the fingers are swollen. The tympanum is visible.

SIMILAR SPECIES: The taxonomic relationships between *P. ukingensis*, *P. mababiensis*, and *P. parvulus* are unclear. *P. mababiensis* lacks distinct toe disks in contrast to *P. ukingensis*.

HABITAT: Montane forest and grassland

NATURAL HISTORY: Assumed to breed in pools and marshes. Eggs are small and black and float on the surface of the water.

CALL: Buzzes and clicks

DISTRIBUTION IN THE EACF: Uluguru, Ukinga and Rungwe Mountains

TYPE LOCALITY: Madehani, Ukinga Mountains, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: above 1000 m

CONSERVATION STATUS: Data deficient

UREFU WA MWILI: ♂ 19 mm; ♀ 21 mm

MAELEZO: Chura hawa ni wadogo sana na wana ngozi laini kahawia na nundu pana. Baadhi ya vyura wana mistari mgongoni ambayo imefifia au mistari kwenye sehemu ya juu na / au mistari miguuni. Madume yana koo jeusi. Mwisho wa vidole vya mguuni kuna ncha mviringo zinazojitokeza. Ncha za vidole vya mkononi vimevimba. Kiwambo cha masikio kinaonekana.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Mahusiano kati ya *P. mababiensis*, *P. parvulus* na *P. ukingensis* hayajajulikana vizuri. Tofauti na *P. ukingensis*, *P. mababiensis* hana ncha mviringo za vidole.

MAZINGIRA: Misitua ni nyika zilizopo 1200 m kutoka usawa wa bahari.


HISTORIA ASILIA: Inadhaniwa spishi hii inazaliana kwenye madimbwi na vinamasi. Mayai ni madogo na meusi na yanaelea juu ya maji.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Milima ya Uluguru, Ukinga na Rungwe

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Madehani, Milima ya Ukinga, Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: > 1000 m

HALI YA UHIFADHI: Hakuna taarifa za kutosha



Phrynobatrachus uzunguensis (Grandison & Howell, 1984)



M. Menegon

SVL: ♂ 21 mm; ♀ 25 mm

DESCRIPTION: A small frog with long legs (tibia greater than $\frac{1}{2}$ SVL). The arms, finger tips and some dorsal markings are red-orange. Fingers and toes have small disks. The tympanum is not clearly visible. Males in breeding condition have small white spines on the dorsum, and dark thumb pads. In both males and females the lower jaw is black, but the throat is white, sometimes with darker mottling.

SIMILAR SPECIES: Similar to *P. rungwenis*, but the throat is white in

P. uzunguensis. *P. uzunguensis* can be distinguished from other members of the genus by its small disks and lack of a visible tympanum.

HABITAT: Streams in montane and submontane forest.

NATURAL HISTORY: Breeding is assumed to take place in streams

CALL: Unknown

DISTRIBUTION IN THE EACF: Udzungwa, Uluguru and Nguu Mountains. Likely occurs in other mountains of the Eastern Arc.

TYPE LOCALITY: Mwanihana Forest Reserve, Udzungwa Mountains, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: Above 900 m

CONSERVATION STATUS: Vulnerable

UREFU WA MWILI: ♂ 21 mm; ♀ 25 mm

MAELEZO: Chura huyu ni mdogo mwenye miguu mirefu (muundi gongo ni zaidi ya $\frac{1}{2}$ ya SVL). Mikono, ncha za kucha za vidole vya mkononi na baadhi ya alama za sehemu ya juu ni nyekundu machungwa. Vidole vya mikononi na miguuni vina ncha mviringo na ndogo. Kiwambo cha sikio hakionekani vizuri. Kwenye msimu wa kupandana, madume yana miiba midogo na mieupe sehemu ya juu na uvimbe mweusi chini ya kidole gumba. Taya ya chini ya madume na majike ni nyeusi lakini koo ni jeupe na wakati mwingine linakuwa na madoa meusi.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Inafanana na *P. rungwenis*, lakini koo la *P. uzunguensis* ni jeupe. Tofauti na spishi zingine za jenasi, *P. uzunguensis* ina ncha za vidole mviringo ndogo na haina kiwambo cha sikio kinachoonekana.

MAZINGIRA: Vijito kwenye misitu karibu au zaidi ya 1200 m kutoka usawa wa bahari.


HISTORIA ASILIA: Inadhaniwa inazaliana kwenye vijito.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Milima ya Udzungwa, Uluguru na Nguu. Huenda inapatikana kwenye milima mingine ya Tao la Mashariki.

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Hifadhi ya Misitu ya Mwanihana, Milima ya Udzungwa, Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: > 900 m

HALI YA UHIFADHI: Inaweza kuathiriwa



Pipidae

The family Pipidae includes two species that can be found in the Eastern Arc and Coastal Forests. Both are in the genus *Xenopus*. These species are fully aquatic, and have flattened stream-lined bodies, small eyes, smooth skin and black claws on the inner three toes.

Familia ya Pipidae inajumuisha spishi mbili ambazo zinapatikana kwenye TMMP kwenye jenasi ya *Xenopus*. Aidha, spishi zote zinaishi majini na zina miili iliyonyooka, macho madogo, ngozi laini na makucha meusi kwenye sehemu ya ndani na vidole vitatu vya mguuni.



Claws of *Xenopus*
J. Vonesh

Xenopus borealis (Parker, 1936)

Northern Clawed Frog



J. Vonesh

SVL: ♂ 50 -60 mm; ♀ 59 - 80 mm

DESCRIPTION: *X. borealis* is a small clawed frog with olive to brown skin, occasionally with darker mottling. The vent can be bright orange which is concentrated in axillary areas with a paler vent, all with black splotches to varying degree of intensity. Lateral lines appear as "stitching" all over the body, but obviously in rings around the eyes. Males develop dark nuptial pads on the arms during breeding periods, females have three cloacal lips which become pink and swollen.

SIMILAR SPECIES: The sub-ocular tentacle of *X. borealis* is much shorter than $\frac{1}{2}$ the diameter of the eye while that of *X. muelleri* is grater than $\frac{1}{2}$ the diameter of the eye.

HABITAT: Permanent ponds in forest or agricultural landscapes. Habitats also include very small wells in which it may fall when dispersing.

NATURAL HISTORY: Breeding activity starts with the onset of heavy rains. Males call from within the water (although the calls can be heard sometimes quite loudly but muffled from outside), and appear to be very territorial getting into wrestling matches with other males. Males clasp females in inguinal amplexus, swimming underwater and depositing eggs singly onto vegetation. Tadpoles are suspension feeders which swim in schools hanging in mid-water with just a flicker at the ends of their tails. They resemble catfish with long tentacles projecting from the corners of their wide mouths.

CALLS: Males call with a series of trills and clicks. Females probably also vocalize in this species.

DISTRIBUTION IN THE EACF: Kenyan highlands and adjoining upland areas of Tanzania.

TYPE LOCALITY: Marsabit, Kenya

ELEVATIONAL RANGE: 600 – 1700 m

CONSERVATION STATUS: Least Concern

UREFU WA MWILI: ♂ 50 – 60 mm; ♀ 59 – 80 mm

MAELEZO: *X. borealis* ni chura mdogo mwenye makucha na ngozi yenye rangi ya mzeituni hadi kahawia, na wakati mwingine anakuwa na madoa madoa meusi. Tundu la kutolea haja na kutoa na kupokelea mbegu za uzazi linaweza kuwa rangi ya machungwa inayong'aa, iliyokolea zaidi kwenye makwapa na madoa meusi ambayo kukolea kwake kunatofautiana. Mistari ya pembeni inaonekana kama imeunganishwa kwa kushona kwenye mwili mzima na inazunguka macho. Wakati wa msimu wa kupandana, madume yanakuwa na ngozi nyeusi inayokwaruza ya kusaidia kukamata majike, majike yanakuwa na vipande vitatu vya ngozi rangi ya waridi na vilivyovimba kwenye eneo la tundu la kutolea haja na kutoa na kupokelea mbegu za uzazi.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Mnyiri chini ya jicho wa *X. borealis* ni mfupi zaidi ya $\frac{1}{2}$ ya kipenyo cha jicho wakati mnyiri wa *X. muelleri* ni zaidi ya $\frac{1}{2}$ ya kipenyo cha jicho.

MAZINGIRA: Madimbwi ya kudumu kwenye misitu au maeneo ya kilimo; aidha, vyura hawa wanapatikana kwenye visima vidogo sana ambapo wanaanguka wanapotawanyika.


HISTORIA ASILIA: Kuzaliana kunaanza mwanzoni mwa mvua kubwa. Madume yanaita yakiwa majini (ingawa miito inaweza kusikika kwa nguvu lakini siyo kutoka nje) na yanalinda sana maeneo yao na hata kupigana miereka na madume mengine. Madume yanakamata majike kutoka miguu ya nyuma wakati wa kupandana, yanaogelea chini ya maji na kupeleka mayai moja moja kwenye uoto. Viluwiluwi vinakula vitu vidogo sana vinavyoelea majini na vinaogelea kwenye makundi, vikiring'inia katikati ya maji; sehemu ndogo sana ya mwishoni mwa mkia ndiyo inaonekana. Vinafanana na kambare mwenye mijiri mirefu inayojitokeza kutoka kona za midomo mipana.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMP: Kusini mwa Kenya na Kaskazini mwa Tanzania.

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Marsabit, Kenya

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: 600 – 1700 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini.



Xenopus muelleri (Peters, 1844)

Yellow-bellied Platanna, Northern Platanna, Müller's Clawed Frog, Savanna Clawed Frog



E. Harper

SVL: ♂ < 50 mm; ♀ < 90 mm

DESCRIPTION: A large aquatic frog. The dorsum is gray with scattered darker blotches, and the ventral surface is light with bright yellow below the legs. Some faint gray shading is often present in the pectoral region. The eyes are small with round pupils and a conspicuous sub-ocular tentacle that is greater than ½ the diameter of the eye. Lateral line organs are clearly visible, appearing as a series of 22 – 27 'stitches' along each side. The toes are fully webbed and the tips of the inner three toes end

in darkly pigmented claws.

SIMILAR SPECIES: The sub-ocular tentacle of *X. borealis* is much shorter than ½ the diameter of the eye while that of *X. muelleri* is greater than ½ the diameter of the eye.

HABITAT: Aquatic habitat in lowland savanna, including permanent and temporary ponds, streams and rivers. Tolerates habitat modification and can be found in agricultural areas.

NATURAL HISTORY: Breeding takes place in muddy pools. The breeding behavior of this species is not well known. It is likely similar to that of other species in the genus in which eggs are attached to submerged rocks or vegetation. The eggs are small and darkly pigmented. Tadpoles are large with long tentacles that are at least ¼ the total length. Tadpoles lack keratinized mouthparts and form schools, feeding on unicellular algae in the water column. All *Xenopus spp.* lack tongues, and feed by sucking in aquatic prey, sometimes with the aid of their long fingers.

CALL: Males call while under water, and lack a visible vocal sac. The call is a series of clicks emitted at a rate of two per second.

DISTRIBUTION IN THE EACF: Throughout the Eastern Arc Mountains, also on the islands of Zanzibar and Mafia.

TYPE LOCALITY: Mozambique

ELEVATIONAL RANGE: Primarily lowland, but may occur up to 2000 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ < 50 mm; ♀ < 90 mm

MAELEZO: Chura huyu ni mkubwa sana na anaishi majini. Sehemu ya juu ni kijivu na ina madoa yenye rangi iliyokolea zaidi hapa na pale na sehemu ya chini ina rangi iliyofifia, isipokuwa chini ya miguu yenye njano inayong'aa. Mara nyingi kuna kijivu kilichofifia kifuani. Macho ni madogo, yana mboni mvingo na mnyiri chini ya jicho ambao ni zaidi ya ½ ya kipenyo cha jicho. Ogani za fahamu zinaonekana kama mfululizo wa mishono 22-27 kila upande. Vidole vya mguuni vina utando na ncha za vidole vitatu vya ndani mguuni zina makucha yenye rangi nyeusi.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Mnyiri chini ya jicho wa *X. borealis* ni mfupi zaidi ya ya kipenyo cha jicho wakati mnyiri wa *X. muelleri* ni zaidi ya ya kipenyo cha jicho

MAZINGIRA: Mazingira ya maji kwenye savana ya maeneo tambarare, pamoja na madimbwi ya kudumu na ya muda, vijito na mito. Inavumilia mazingira yaliyobadilika na inapatikana kwenye maeneo ya kilimo.

HISTORIA ASILIA: Inazaliana kwenye madimbwi yenye tope. Mfumo wake wa kuzaliana haujulikani vizuri na inadhaniwa unafanana na wa spishi zingine za jenasi ambapo mayai yanagandishwa kwenye miamba au uoto chini ya maji. Mayai ni madogo na meusi sana. Viluwiluwu ni virefu na vina minyiri yenye urefu ambao ni angalau ¼ ya urefu mzima. Aidha, viluwiluwu havina sehemu maalum kwa ajili ya kula uoto wa majini na vinakuwa kwenye makundi na kula mwani wenye seli moja. *Xenopus spp* wote hawana ulimi na wanakula kwa kufyonza chakula, wakati mwingine kwa kutumia vidole virefu vya mkononi.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP:

Maeneo yote ya MTMMP ya Tanzania na Kenya na visiwa vya Zanzibar na Mafia.


MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA

MARA YA KWANZA: Msumbiji

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI:

Maeneo tambarare lakini inaweza kupatikana hadi kwenye 2000 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Ptychadenidae

Until recently, the species in this family were considered to be in the family Ranidae. Ptychadenidae consists of three genera, with the majority of species in the genus *Ptychadena*. Species in two genera, *Hildebrandtia* and *Ptychadena*, can be found in the Eastern Arc and Coastal Forests. *Hildebrandtia ornata* is a stocky burrowing frog with short legs. The *Ptychadena* species, in contrast, typically have streamlined bodies with long legs and are excellent jumpers. They are notoriously difficult to catch and are often referred to as “rocket frogs”.

Mpaka hivi karibuni, spishi katika familia hii zilikuwa zimeingizwa kwenye familia ya Ranidae. Ptychadenidae ina jenasi tatu na idadi kubwa ya spishi ziko kwenye jenasi ya *Ptychadena*. Spishi katika jenasi mbili za *Hildebrandtia* na *Ptychadena* zinapatikana kwenye TMMP. *Hildebrandtia ornata* ni chura mnene, ana miguu mifupi na anachimba mashimo ardhini. Lakini spishi za *Ptychadena* zina miili iliyoonyoka, miguu mizuri na zinaruka vizuri sana. Ni vigumu sana kuwakamata vyura hawa na mara nyingi wanajulikana kama “vyura roketi”



Ptychadena
E. Harper

Hildebrandtia ornata (Peters, 1878)

Ornate Pyxie, Black-throated Pyxie, Ornate Burrowing Frog,
Hildebrandt's Burrowing Frog



A. Channing

SVL: ♂ 44 – 49 mm; ♀ < 45 mm

DESCRIPTION: A plump looking frog with warty and folded skin, prominent eyes and short legs. The color pattern on the dorsum can be striking to dull with combinations of yellow brown to olive green with dark mottling on the sides. The ventrum is white to cream. Males have dark spots or mottling on the throat and paired lateral vocal sacs.

SIMILAR SPECIES: Similar body shape to *Pyxicephalus edulis*, but *H. ornata* lacks the teeth-like projections on the jaw.

HABITAT: Savanna, especially in areas with sandy soil.

NATURAL HISTORY: A fossorial species that comes above ground only during the breeding season. Breeding takes place in temporary pools that lack vegetation. Males call from the water's edge. Single eggs are scattered by the female during amplexus, typically during the beginning of the rainy season.

CALL: A short "hoot"

DISTRIBUTION IN THE EACF: Throughout the Eastern Arc Mountains in Kenya and Tanzania and in coastal areas of Tanzania. Its distribution is patchy within its range due to its habitat requirements.

TYPE LOCALITY: Taita, Kenya

ELEVATIONAL RANGE: < 1200 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ 44 – 49 mm; ♀ < 45 mm

MAELEZO: Chura huyu ni mnene, ana ngozi yenye chunjuwa na mkunjo kwenye ngozi, macho makubwa na miguu mifupi. Mpangilio wa rangi sehemu ya juu ni wa kuvutia au hapana, ni mchanganyiko wa kahawia, njano, hadi kijani mzeituni na madoa pembeni. Aidha, chura hawa ni weupe sehemu ya chini na madume yana madoa meusi au madoa yenye rangi mbalimbali kwenye koo na vifuko ya sauti viwili viwili.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Umbile la mwili linafanana na la *Pyxicephalus edulis* lakini *H. ornata* hana sehemu iliyochochoza kama meno kwenye taya

MAZINGIRA: Savana, hasa kwenye maeneo yenye udongo wa mchanga.


HISTORIA ASILIA: Spishi hii inachimba mashimo ardhini na kuishi humo muda mwingi na inajitokeza juu ya ardhi msimu wa kuzaliana tu. Inazaliana kwenye madimbwi ya muda bila uoto na madume yanaita kutoka pembeni mwa madimbwi. Jike linataga mayai, dume linaweka mbegu zake kwenye mayai yanapotoka nje ya jike, ambalo huyatawanya moja moja.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Maeneo yote ya MTMMP ya Tanzania na Kenya.

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Taita, Kenya

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: < 1200 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Ptychadena anchietae (Bocage, 1867)

Plain Grass Frog, Savanna Ridged Frog, Anchieta's Ridged Frog, Long-legged Grass Frog



E. Harper

SVL: ♂ < 51 mm; ♀ < 62 mm

DESCRIPTION: A medium-sized frog with long legs. The dorsum is uniform brown with around 7 rows of parallel ridges. Some individuals have darker blotches scattered over the dorsum. Middorsal and tibial stripes are never present. A distinct pale triangle covers the area of the snout in front of the eyes. The tympanum is clearly visible and edged in white. The toes are nearly fully webbed, with only the tip of the fourth toe free of webbing.

SIMILAR SPECIES: *P. anchietae* can be

distinguished from other members of the genus by the pale triangle on the snout, horizontal stripes on the backs of the thighs, and extensive toe webbing with only the last joint of the longest toe free of webbing.

HABITAT: Open areas in lowland savannas, grasslands and woodlands. Tolerates some habitat modification and may be found in former forest, agricultural and suburban areas. Typically found near water.

NATURAL HISTORY: Small eggs, gray on top and white below, are laid in a single layer that floats on the surface of the water. Tadpoles are brown above and light below with a clear fin and may reach 45 mm in length.

CALL: Males call near the edge of temporary pools and flooded grasslands. The call is a rapid high-pitched trill repeated three times every two seconds.

DISTRIBUTION IN THE EACF: Throughout Kenya and Tanzania

TYPE LOCALITY: Benguela, Angola

ELEVATIONAL RANGE: < 1800 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ < 51 mm; ♀ < 62 mm

MAELEZO: Chura huyu ana saizi ya kati na miguu mirefu. Sehemu yote ya juu ni kahawia na ina takribani safu 7 za matuta sambamba. Baadhi ya vyura wana madoa meusi yaliyotapakaa sehemu ya juu. Hakuna mistari ya juu katikati ya mgongo wala muundi goko. Pembetatu iliyofifia inafunika eneo la pua na mbele ya macho. Kiwambo cha sikio kinaonekana na pembeni kina rangi nyeupe. Karibu vidole vyote vya mguu vina utando isipokuwa ncha ya kidole cha tano.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Tofauti ya *P. anchietae* na spishi zingine za jenasi ni kwamba ina pembetatu yenye rangi ya kufifia kwenye pua, mistari mlalo nyuma ya mapaja na utando mwingi kwenye vidole vya mguuni isipokuwa kifundo cha kidole kirefu kuliko vyote ambacho hakina kabisa.

MAZINGIRA: Maeneo wazi na tambarare ya savana, nyika na miombo. Inavumilia mazingira yaliyobadilika kidogo na inapatikana palipokuwa na misitu awali, maeneo ya kilimo na viunga vya miji. Inapatikana karibu na maji.


HISTORIA ASILIA: Mayai madogo ambayo ni kijivu juu na meupe chini yanatagwa kwenye tabaka moja linaloelea juu ya maji. Viluwiluwi ni kahawia juu na rangi iliyofifia chini na vina pezi angavu na vinaweza kufikia urefu wa 45 mm.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Maeneo yote ya Kenya na Tanzania

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Benguela, Angola

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: < 1800 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Ptychadena grandisonae (Laurent, 1954)
Muita Grassland Frog, Grandison's Ridged Frog



A. Channing

SVL: ♀ < 44 mm; ♂ < 50 mm

DESCRIPTION: A medium-sized frog with long legs. The dorsum has dark spots and raised parallel ridges, but the ridges do not extend onto the snout. There is usually a light middorsal stripe. The tympanum is distinctly visible with a light dot in the center. There is no light line on the tibia. There are spots rather than bands on the back of the thighs. Three joints of the fourth toe are free of webbing.

SIMILAR SPECIES: Multiple characteristics are necessary to

distinguish *P. grandisonae* from other members of the genus. The back of the thigh is mottled, in contrast to the horizontal or vertical bands of several of the other species in the genus. *P. grandisonae* lacks ridges on the snout, does not have a pale triangle on the snout, and has long legs (tibia longer than $\frac{1}{2}$ SVL).

HABITAT: High elevation savannas and grassland

NATURAL HISTORY: Breeding takes place in wet grassy areas.

CALL: Channing (2001) describes the call as a "slow rising 'wauk'"

DISTRIBUTION IN THE EACF: Udzungwa Mountains

TYPE LOCALITY: Muita, Luembe, Angola

ELEVATIONAL RANGE: < 1900 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♀ < 44 mm; ♂ < 50 mm

MAELEZO: Chura huyu ana saizi ya kati na miguu mirefu. Sehemu ya juu ina madoa meusi na matuta sambamba yaliyoinka, lakini matuta hayafiki puani. Kwa kawaida, kuna mstari uliofifia katikati ya mgongo. Kiwambo cha sikio kinaonekana na katikati, kina doa lililofifia. Hakuna mstari uliofifia kwenye muundi goko. Nyuma ya mapaja, kuna madoa na siyo mistari. Viungo vitatu vya kidole cha nne cha miguuni havina utando.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Sifa nyingi zinaitofautisha *P. grandisonae* na spishi zingine za jenasi. Sehemu ya nyuma ya mapaja ina mchanganyiko wa rangi, tofauti na mistari wima au mlalo ya spishi kadhaa za jenasi. *P. grandisonae* haina matuta wala pembetatu kwenye pua na ina miguu mirefu.

MAZINGIRA: Savana na nyika kwenye miinuko ya juu


HISTORIA ASILIA: Inazaliana kwenye maeneo yenye nyasi zenye unyevu

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Milima ya Udzungwa

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Muita, Luembe, Angola

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: < 1900 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Ptychadena mascareniensis (Duméril & Bibron, 1841)

Mascarene Grass Frog, Broad-banded Ridged Frog, Mascarene Rocket Frog



G.J. Measey

SVL: ♂ 38 – 48 mm; ♀ 48 – 66 mm

DESCRIPTION: A medium-sized greenish brown frog with long legs and several rows of parallel ridges on the dorsum. There are several dark squarish markings on the dorsum and additional markings that can vary in color including reds, greens and yellows. The snout is long and pointed and the nostrils are nearer to the snout than to the eyes. The tympanum is visible, usually with a light mark in the center, and is slightly smaller than the diameter of the eye. A light middorsal stripe is usually present, as well as a thin light

line on the tibia. There is a distinct light stripe on the upper lip. The ventral surface is smooth and light without mottling. The last two joints of the longest toe are free of webbing. The back of the thighs are mottled yellow or green and black, but lack distinct stripes or large spots.

SIMILAR SPECIES: *P. mascareniensis* likely contains at least 5 cryptic species. This species can be distinguished from other members of the genus by the horizontal stripes on the backs of the thighs, the lack of a pale triangle on the snout and the extent of toe webbing.

HABITAT: Wet lowland areas in humid savanna and agricultural areas. Also common in roadside ditches in forest.

NATURAL HISTORY: Breeding takes place in pools, ditches and tire ruts. Small black and white eggs are laid in shallow water. Tadpoles are small and metamorphose after nine weeks.

CALL: Males call from the water's edge or while propped on aquatic vegetation. The call is described as "a series of clucking sounds, repeated rapidly," by Channing (2001).

DISTRIBUTION IN THE EACF: Throughout the Eastern Arc and Coastal Forests of Kenya and Tanzania, also on Mafia Island

TYPE LOCALITY: Réunion and Mascarene Islands, Indian Ocean [although Réunion populations were likely introduced]

ELEVATIONAL RANGE: 0 – 2000 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ 38 – 48 mm; ♀ 48 – 66 mm

MAELEZO: Chura huyu ana saizi ya kati, ni kijani-kahawia, ana miguu mirefu na safu kadhaa za matuta sambamba kwenye sehemu ya juu. Aidha, kuna alama nyeusi za mraba kwenye sehemu ya juu na alama zingine zinazotofautiana rangi, zikiwepo nyekundu, kijani na njano. Pua ni ndefu na imechongoka; matundu ya pua yako karibu zaidi na pua kuliko macho. Kiwambo cha sikio kinaonekana na kwa kawaida, kina alama iliyofifia katikati na ni kidogo kuliko kipenyo cha jicho. Kuna mstari wenye rangi iliyofifia na unaojitokeza vizuri kwenye mdomo wa juu. Sehemu ya chini ni laini, ina rangi iliyofifia na haina madoa. Viungo viwili vya mwisho vya kidole cha mguuni virefu kuliko vyote havina utando. Sehemu ya nyuma ya mapaja ina mistari sambamba isiyokuwa na mpangilio. Kuna mstari uliofifia kwenye miguu.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: *Ptychadeni mascareniensis* ina angalau spishi 5 ambazo bado hazijaainishwa. Tofauti ya spishi hii na zingine kwenye jenasi ni kwamba ina mistari mlalo sehemu ya nyuma ya mapaja, haina pembetatu kwenye pua na kuenea kwa utando kwenye vidole vya mguu ni tofauti pia.

MAZINGIRA: Maeneo tambarare yenye unyevu kwenye savana na maeneo ya kilimo. Inapatikana sana pia kwenye madimbwi kando kando ya barabara misituni.

HISTORIA ASILIA: Inazaliana kwenye madimbwi na matairi. Mayai madogo meusi na meupe yanatagwa kwenye maji ya kina kifupi. Viluwiluwi ni vidogo na vinamaliza hatua zote za mabadiliko baada ya majuma tisa.


ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP:

Maeneo yote ya MTMMP ya Tanzania na Kenya na kwenye kisiwa cha Mafia

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Réunion na Mascarene

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: 0 – 2000 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Ptychadena mossambica (Peters, 1854)

Single-striped Grass Frog, Broad Banded Grass Frog,
Mozambique Grass Frog



SVL: ♂ 29 – 35 mm; ♀ 33 – 44 mm

DESCRIPTION: The dorsum is brown or olive green with dark spots and a wide pale middorsal stripe. The parallel ridges on the dorsum are continuous rather than interrupted. The snout is sharply pointed. There is no light spot on the tympanum. Unlike most of the frogs in this genus, the tibia is less than ½ the SVL. Three sections of the longest toe are free of webbing. The back of the thigh is mottled without distinct stripes or large spots. Some individuals have a light line on the tibia.

SIMILAR SPECIES: *P. mossambica* can be distinguished from other members of the genus by its shorter legs (tibia equal to or less than ½ SVL).

HABITAT: Dry grassland, shrubland and savanna

NATURAL HISTORY: Breeding takes place in temporary pools and flooded grassland

CALL: Pickersgill (2007) describes the call as “a nasal honk”

DISTRIBUTION IN THE EACF: Throughout the Eastern Arc Mountains and Coastal Forest of Kenya and Tanzania

TYPE LOCALITIES: Tete, Mozambique

ELEVATIONAL RANGE: 200 – 1200 m (possibly higher)

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ 29 – 35 mm; ♀ 33 – 44 mm

MAELEZO: Sehemu ya nyuma ni kahawia au rangi ya mzeituni, kuna madoa meusi na katikati, msitari mpana uliofifia. Kuna matuta sambamba kwenye sehemu ya juu ambayo ni mfululizo, hayajakatika. Pua imechongoka sana. Hakuna doa lililofifia kwenye kiwambo cha sikio. Tofauti na vyura wengi wa jenasi hii, muundi goko ni chini ya ½ ya SVL. Sehemu tatu za kidole cha mguuni hazina utando. Sehemu ya nyuma ya paja ina madoa madogo lakini haina mistari wala madoa makubwa. Baadhi ya vyura wana mstari uliofifia kwenye muundi goko.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Tofauti na spishi zingine za jenasi, *Ptychadena mossambica* ina miguu mifupi zaidi (muundi goko ni au chini ya ½ ya SVL)

MAZINGIRA: Nyika kame, vichaka na savanna

HISTORIA ASILIA: Inazaliana kwenye madimbwi ya muda na nyika zinazofurika maji

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Maeneo yote ya MTMMP ya Tanzania na Kenya

TYPE LOCALITIES: Tete, Mozambique

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: 200 – 1200 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Ptychadena oxyrhynchus (Smith, 1849)

Shrarp-snouted Ridged Frog, Sharp-nosed Grass Frog, Sharp-nosed Rocket Frog



E. Harper

SVL: ♂ < 42 - 62 mm; ♀ 58 - 85 mm

DESCRIPTION: A medium-sized frog with very long legs and an acutely sharp snout. The dorsum is brown, often with dark spots, and with several rows of parallel ridges. Some individuals also have bright orange markings. There is a pale triangle on the snout. Distinct, light dorsolateral folds are clearly visible. There is a light stripe on the upper lip that extends below the eye and the tympanum. The tympanum is clearly visible and has a light dot at the center. The nostrils are closer to the tip of the snout than to the

eyes. The ventral surface is smooth and light, sometimes with yellowing toward the groin. Toes are extensively webbed, with only the last one or two joints of the longest toe free of webbing. The back of the thighs are mottled yellow or green and black, but lacks distinct stripes or large spots.

SIMILAR SPECIES: *P. anchiete* and *P. oxyrhynchus* both have a pale triangle on the snout, but *P. anchiete* has horizontal stripes on the posterior surface of the thigh rather than mottling as in *P. oxyrhynchus*.

HABITAT: Wet areas of savanna, agricultural areas and degraded forest.

NATURAL HISTORY: Small brown and white eggs are deposited in small temporary pools, ditches and ruts in clutches as large as 3500. Eggs are laid in short strings which later break apart allowing eggs to float singly on the surface of the water. Tadpoles are gray with a pale head and a clear tail with scattered dark spots. Tadpoles are up to 54 mm in length.

CALL: Males call from the ground, sometimes but not always near water. The call is a long sharp trill.

DISTRIBUTION IN THE EACF: Throughout the Eastern Arc and Coastal Forest

TYPE LOCALITY: Durban, South Africa

ELEVATIONAL RANGE: < 2000 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ < 42 - 62 mm; ♀ 58 - 85 mm

MAELEZO: Chura huyu ana saizi ya kati, miguu mirefu sana na pua iliyochongoka sana. Sehemu ya juu ni kahawia na mara nyingi ina madoa meusi na safu kadhaa za matuta sambamba. Baadhi ya vyura wana alama za rangi ya machungwa inayong'aa. Kuna pembetatu iliyofifia kwenye pua. Makunjo yenye rangi iliyofifia yanaonekana katikati ya mgongo. Kuna mstari uliofifia kwenye mdomo wa juu unaopita chini ya jicho na kiwambo cha sikio. Kiwambo cha sikio kinaonekana vizuri na kina doa lililofifia sehemu ya katikati. Matundu ya pua yako karibu zaidi na ncha ya pua kuliko na macho. Sehemu ya chini ni laini na ina rangi iliyofifia, na wakati mwingine njano njano karibu na kinena. Vidole vya miguuni vina utando sehemu kubwa; kiungo kimoja au viwili tu vya kidole kirefu kuliko vyote hakina utando. Sehemu ya mwisho ya mapaja ina madoa njano, kijani au meusi lakini haina mistari au madoa makubwa.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: *P. anchiete* na *P. oxyrhynchus* zina pembetatu zenye rangi iliyofifia kwenye pua, lakini *P. anchiete* ina mistari mlalo sehemu ya mbele ya paja na siyo madoa kama ilivyo kwa *P. oxyrhynchus*

MAZINGIRA: Maeneo ya savana yenye unyevu, maeneo ya kilimo na misitu iliyoharibiwa.


HISTORIA ASILIA: Mayai madogo kahawia na meupe yanatagwa kwenye madimbwi madogo, mifereji na matairi; vyura wanataga mayai kwenye makundi yenye mayai 3500, kwenye mistari mifupi ambayo baadaye inakatika na kuacha mayai yakielea moja moja juu ya maji. Viluwilwi ni kijivu na vina vichwa vyenye rangi iliyofifia na mkia angavu wenye madoa meusi. Urefu wa viluwilwi unafikia 54 mm.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Maeneo yote ya MTMMP ya Tanzania na Kenya.

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Durban, Afrika ya Kusini

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: < 2000 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Ptychadena taenioscelis (Laurent, 1954)

Stripe-legged Frog, Dwarf Grass Frog, Spotted Throated Ridged Frog, Lukula Grassland Frog, Small Ridged Frog



G.J. Measey

SVL: ♂ < 35 mm; ♀ < 40 mm

DESCRIPTION: A small to medium-sized frog with long legs and a pointed snout. The dorsum is brown with darker squarish markings. There are raised parallel ridges on the dorsum, and two of the ridges extend between the eyes onto the snout. The tympanum is clearly visible, smaller than the eye and has a light dot at the center. The nostrils are closer to the tip of the snout than to the eyes. A light ridge of skin runs from the tip of the snout under the eye and tympanum to the base of the

arm. Raised dorsolateral folds may be red or yellowish in color. A thin light line typically runs from the tip of the snout to the vent. There may also be a thin light line on the tibia. The backs of the thighs have distinct vertical stripes. The legs are darkly barred. Toes are partially webbed, but three sections of the longest toe are free of webbing.

SIMILAR SPECIES: The distinct vertical bands on the backs of the thighs and the pair of ridges on the snout distinguish this species from others in the genus.

HABITAT: Grasslands and savanna woodland

NATURAL HISTORY: Breeding takes place in shallow pools and flooded grassland

CALL: The advertisement call is described by Channing and Howell (2006) as “a rapid chirp” with each call consisting of “22 – 25 rapid pulses”

DISTRIBUTION IN THE EACF: Coastal Tanzania and in the Eastern Arc Mountains from the Ukagurus south to the Udzungwa Mountains

TYPE LOCALITY: Lukula, Democratic Republic of Congo

ELEVATIONAL RANGE: Unclear

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ < 35 mm; ♀ < 40 mm

MAELEZO: Chura huyu ana saizi ndogo hadi kubwa kiasi, miguu mirefu na pua iliyochoongoka. Sehemu ya mgongoni ni kahawia na ina alama ya mraba mweusi. Kuna matuta sambamba yaliyoinuka kwenye sehemu ya chini na matuta mawili yanatoka katikati ya macho hadi kwenye pua. Kiwambo cha sikio kinaonekana vizuri, ni kidogo kuliko jicho na kina doa lililofifia katikati. Matundu ya pua yako karibu zaidi ya ncha ya pua kuliko macho. Tuta la ngozi lililofifia linatoka ncha ya pua chini ya jicho, linapita kiwambo cha sikio hadi mwanzoni mwa mkono. Makunjo yaliyoinuka ya katikati ya mgongo ni mekundu au njano njano. Mstari mwembamba uliofifia unatoka ncha ya pua hadi kwenye tundu la kutolea haja na kutoa na kupokelea mbegu za uzazi. Inawezekana pia kukawa na mstari mwembamba uliofifia kwenye muundi goko. Sehemu ya nyuma ya mapaja ina mistari wima inayoonekana vizuri. Miguu ina mistari mieusi. Vidole vya miguuni vina utando kiasi lakini sehemu tatu za kidole kirefu kuliko vyote hazina utando.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: *Ptychadena* spishi

MAZINGIRA: Tofauti na spishi zingine za jenasi, spishi hii ina mistari wima nyuma ya mapaja na matuta mawili mawili kwenye pua.

HISTORIA ASILIA: Inazaliana kwenye madimbwi yenye kina kifupi na nyika zilizofurika maji.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Pwani ya Tanzania na Milima ya Tao la Mashariki kuanzia Ukaguru kuelekea kusini hadi Milima ya Udzungwa

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Lukula, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Ptychadena uzungwensis (Loveridge, 1932)
Udzungwa Ridged Frog, Udzungwa Grassland Frog



A. Channing

SVL: ♂ < 42 mm; ♀ < 48 mm

DESCRIPTION: A medium-sized frog with parallel ridges on the dorsum that are broken rather than continuous. The dorsal color is dark brown with darker brown spots. There are two distinct ridges on the snout. Light dorsolateral folds of skin run along each side of the body. There is a light middorsal stripe. The back of the thigh is faintly spotted and in some individuals the spots join to form a horizontal band. Three joints of the longest toe are free of webbing. Males have yellow throats and yellow patches near the groin.

SIMILAR SPECIES: *P. uzungwensis* has a pair of ridges on the snout and the backs of the thighs are not striped distinguishing this species from others in the genus.

HABITAT: Wet grasslands at moderate to high elevations

NATURAL HISTORY: Breeding takes place in shallow water

CALL: The call is a trill

DISTRIBUTION IN THE EACF: Udzungwa Mountains

TYPE LOCALITY: Dabaga, Udzungwa Mountains, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: 800 – 2300 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ < 42 mm; ♀ < 48 mm

MAELEZO: Chura huyu ana saizi ya kati; sehemu ya juu kuna matuta sambamba ambayo yamekatika na siyo mfululizo. Sehemu ya juu ni kahawia na ina madoa kahawia iliyokolea zaidi. Kuna matuta mawili yanayoonekana vizuri kwenye pua. Kuna makunjo mgongoni na pembeni. Kuna mstari uliofifia katikati ya mgongo. Sehemu ya nyuma ya paja ina madoa yaliyofifia na kwenye baadhi ya vyura, madoa yameungana na kutengeneza mstari mlalo. Vifundo vitatu vya kidole cha mguuni virefu kuliko vyote na havina utando. Madume yana koo na madoa njano karibu na kinena.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Tofauti na spishi zingine za jenasi, *Ptychadena uzungwensis* ina matuta mawili kwenye pua na hakuna mistari nyuma ya mapaja.

MAZINGIRA: Nyika zenye unyevu kwenye miinuko ya kati hadi ya juu


HISTORIA ASILIA: Inazaliana kwenye maji ya kina kifupi

ENE SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Milima ya Udzungwa

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Dabaga, Milima ya Udzungwa, Tanzania

ENE LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: 800 – 2300 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Pyxicephalidae

The family Pyxicephalidae includes genera that until recently were considered to be in the family Ranidae. In the Eastern Arc and Coastal Forests, these genera include *Amietia*, *Strongylopus* and *Pyxicephalus*. Several species have historically been lumped under the name *Amietia angolensis*, (previously referred to as *Rana angolensis* or *Afrana angolensis*). Pickersgill (2007) recently removed two Eastern Arc species, *Amietia tenuoplicata* and *Amietia viridireticulata* from this species complex; however more work is still needed. The remaining two genera in this family are each represented by a single species, *Strongylopus fuelleborni* and *Pyxicephalus edulis*.

Familia ya Pyxicephalidae inajumuisha jenasi ambazo mpaka hivi karibuni zilikuwa kwenye familia ya Ranidae. Jenasi zilizopo kwenye MTMMP ni pamoja na *Amietia*, *Strongylopus* na *Pyxicephalus*. Kwa muda mrefu, spishi kadhaa zilipewa jina la *Amietia angolensis*, (kabla ya hapo zilijulikana kama *Rana angolensis* au *Afrana angolensis*). Hivi karibuni, Pickersgill (2007) aliondoa spishi mbili za Tao la Mashariki, *Amietia tenuoplicata* na *Amietia viridireticulata* kutoka kundi hili lakini bado kuna haja ya kufanya utafiti zaidi. Miongoni mwa jenasi mbili zilizobaki kwenye familia, kila moja ina spishi moja tu, *Strongylopus fuelleborni* na *Pyxicephalus edulis*.



Pyxicephalus edulis
R. Drewes

Amietia angolensis (Bocage, 1866)

Common River Frog, Angola River Frog, Dusky-throated Frog



E. Harper

This species is widespread and is almost certainly a complex of multiple cryptic species. *A. tenuoplicata* and *A. viridireticulata* were recently split from *A. angolensis* by Pickersgill (2007). However the ranges of these new species are unknown and it may be that all of the species formerly called *A. angolensis* in the EACF fall under one of these two names. Alternately there may be additional species that will be split from *A. angolensis* in the future. Because the type locality of *A. angolensis* is in Angola it is likely that once the taxonomy is better understood there will no longer be

any species in the EACF called *A. angolensis*. Clearly more work is needed.

SVL: ♀ < 90 mm

DESCRIPTION: A large frog with long legs. The dorsal color and markings are variable, usually browns, greens and yellows, sometimes with darker marks. Dorsal texture is also variable, from smooth to ridged. The tympanum is visible and slightly larger than ½ the diameter of the eye. A fold of skin curves from the eye to the arm over the tympanum. Toes are webbed, usually with only the last section of the longest toe free of webbing, but webbing is variable among populations.

HABITAT: A widespread species in forest, grassland, savanna and agricultural areas. Associated with permanent water.

NATURAL HISTORY: Eggs are laid in shallow water in ponds on the edges of streams in forest and in open areas. The large tadpoles are brown with some flecking, and can reach a total length of 80 mm or greater.

CALL: Males call from the water's edge, often partially submerged. Two different calls, usually emitted in succession, consist of a rattle and a brief croak.

DISTRIBUTION IN THE EACF: Unclear given current taxonomic revisions, but widespread

TYPE LOCALITY: "Duque de Bragança", Angola

ELEVATIONAL RANGE: < 2800 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

Spishi hii imeenea mahali pengi na ni wazi kwamba inajumuisha spishi nyingi zinazofanana ambazo bado hazijaainishwa. *A. tenuoplicata* na *A. viridireticulata* ziliondolewa na Pickersgill (2007) hivi karibuni kwenye spishi ya *A. angolensis*. Hata hivyo, bado spishi hizi mpya hazijajulikana vizuri na inawezekana kwamba spishi zote ambazo awali zilikuwa zinaitwa *A. angolensis* kwenye MTMMP zikawekwa chini ya jina moja kati ya haya mawili. Inawezekana pia zikawepo spishi zingine ambazo zinaweza kuondolewa kwenye *A. angolensis* katika siku zijazo. Kwa vile eneo inakopatikana *A. angolensis* liko Angola, inawezekana kwamba baada ya kuainisha vizuri spishi hizi, huenda kusiwepo spishi zozote kwenye MTMMP zinazoitwa *A. angolensis*. Ni wazi kwamba kuna haja ya kufanya utafiti zaidi.

UREFU WA MWILI: < 90 mm

MAELEZO: Chura huyu ni mkubwa na ana miguu mirefu. Rangi ya sehemu ya juu na alama inatofautiana lakini kwa kawaida ni kahawia, kijani na njano na wakati mwingine yanakuwepo madoa meusi pia. Sehemu ya juu inatofautiana pia, inaweza kuwa laini hadi kuwa na matuta. Kiwambo cha sikio kinaonekana na kinazidi kidogo ½ ya kipenyo cha jicho. Mkunjo wa ngozi unaanzia kwenye jicho, unapita juu ya kiwambo cha sikio hadi mkononi. Vidole vya mguuni vina utando, kwa kawaida ni sehemu moja tu ya kidole cha mguu kirefu kuliko vyote ambayo haina utando, lakini utando unatofautiana kati ya vyura.

MAZINGIRA: Inapatikana kwenye mazingira mengi kama misituni, nyika, savana na maeneo ya kilimo, kwenye maji ya kudumu.

HISTORIA ASILIA: Mayai yanatagwa kwenye madimbwi yenye kina kifupi kando kando ya vijito msituni na maeneo wazi. Viluwiluwi ni wakubwa, kahawia na wana madoa madogo, na wanaweza kufikia urefu wa 80 mm au zaidi.


ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP:

Bado haijulikani kutokana na marekebicho ya uainishaji yanayoendelea, lakini inapatikana mahali pengi

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: "Duque de Bragança", Angola

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: < 2800 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini





SVL: ♀ 57 - 87 mm; males smaller

DESCRIPTION: A large frog with long legs and distinct dorsolateral folds. The dorsum is smooth and brown, often with dark spots. There is a dark line from the snout to the eye that continues as a larger band from the eye, over the tympanum to the corner of the mouth. A light fold of skin extends from the eye over the tympanum to the base of the arm. The tympanum is visible and slightly smaller than the eye. Toe tips are not expanded. The tibia is slightly longer than $\frac{1}{2}$ SVL. The second finger is shorter than the first. One to two segments of the fourth toe are unwebbed. The ventral surface is light, sometimes with dark mottling on the throat. Males in breeding condition have darkly pigmented nuptial pads.

HABITAT: Forest streams

NATURAL HISTORY: Eggs are laid on the edges of streams. Larvae hatch and develop in the water.

CALL: Unclear

DISTRIBUTION IN THE EACF: Currently known only from the type locality, however additional research will likely find that this species is more widespread.

TYPE LOCALITY: Amani, East Usambaras, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: 750 – 1000 m

CONSERVATION STATUS: Data deficient

UREFU WA MWILI: ♀ 57 – 87 mm

MAELEZO: Chura huyu ni mkubwa sana, ana miguu mirefu na mikunjo mgongoni na pembeni inayoonekana. Sehemu ya juu ni laini na kahawia, na mara nyingi ina madoa meusi. Kuna mstari mweusi kutoka puani hadi kwenye macho na unaendelea kama mstari mpana kutoka machoni, kupitia kiwambo cha sikio hadi kwenye kona ya mdomo. Mkunjo wa ngozi uliofifia unatoka jichoni, unapita kwenye kiwambo cha sikio hadi mwanzoni mwa mkono. Kiwambo cha sikio kinaonekana na kidogo kiasi kuliko jicho. Ncha za vidole vya mguuni siyo pana. Miguu ni mirefu kidogo zaidi ya $\frac{1}{2}$ ya SVL. Kidole cha pili cha mkononi kifupi kuliko cha kwanza. Sehemu moja au mbili za kidole cha nne cha mguuni hazina utando. Sehemu ya chini ina rangi iliyofifia na wakati mwingine kuna madoa meusi kwenye koo. Madume yakiwa kwenye msimu wa kupandana yanakuwa na maeneo magumu meusi ya ngozi yanayotumika kumkamata jike.

MAZINGIRA: Vijito vya msituni

HISTORIA ASILIA: Mayai yanatagwa pembeni mwa vijito. Lava wanatolewa na kukua majini.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Kwa sasa, inapatikana tu mahali kielelezo kilipopewa jina kwa mara ya kwanza; lakini utafiti zaidi unaweza kuonyesha kwamba spishi imeenea mahali pengi

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Amani, Milima ya Usambara Mashariki, Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: 750 – 1000 m

HALI YA UHIFADHI : Hakuna taarifa za kutosha





SVL: ♂ 41 – 81 mm; ♀ < 50 - 90 mm

DESCRIPTION: A large brown to olive green frog with irregular darker markings on the dorsum. The dorsal pattern and color can vary. The snout is pointed in profile. Some individuals have a light vertebral stripe. Dorsolateral folds are distinct. There are raised glands scattered along the sides. There is a light stripe above the lip and a dark mask that runs from the tip of the snout, under the eye and over the tympanum. Toes are extensively webbed, with at most one joint of the longest toe free of webbing.

HABITAT: Streams in forest and montane grassland.

NATURAL HISTORY: Eggs are laid on the edges of streams. Larvae hatch and develop in the water.

CALL: Unclear

DISTRIBUTION IN THE EACF: Udzungwa Mountains

TYPE LOCALITY: Dabaga, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: 1740 – 2000 m

CONSERVATION STATUS: Data deficient

UREFU WA MWILI: ♂ 41 – 81 mm; ♀ < 50 – 90 mm

MAELEZO: Chura huyu ni mkubwa, ana rangi ya kahawia hadi kijani ya mzeituni na ana alama nyeusi sehemu ya chini. Kuna tofauti kwenye mpangilio wa sehemu ya juu na rangi. Pua imechongoka. Baadhi ya vyura wana mstari uliofifia mgongoni. Mikunjo ya mgongoni na pembeni inaonekana. Kuna tezi zilizoinuka kila upande. Kuna mstari uliofifia juu ya mdomo na barakoa nyeusi kutoka ncha ya pua, chini ya macho na juu ya kiwambo cha sikio. Vidole vya miguuni vina utando mwingi na angalau kifundo kimoja cha kidole kirefu kuliko vyote vya mguuni hakina utando.

MAZINGIRA: Vijito vya msituni na nyika zilizopo 1200 m kutoka usawa wa bahari

HISTORIA ASILIA: Mayai yanatagwa pembeni mwa vijito. Lava wanatotolewa na kukua majini.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Milima ya Udzungwa

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Dabaga, Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: 1740 – 2000 m

HALI YA UHIFADHI: Hakuna taarifa za kutosha



Strongylopus fuelleborni (Nieden, 1911)

Long-toed Grass Frog, Fülleborn's Stream Frog



E. Harper

SVL: ♂ < 40 mm; ♀ < 53 mm

DESCRIPTION: A slender, long-legged frog with extremely long toes. The snout is pointy. A dark line runs from the snout to the eye and continues under the eye, across the tympanum to the base of the arm. A pale stripe runs from below the eye to the arm under the dark band. There is a pair of distinct skin ridges that begin behind the eye and run to the vent. These ridges are outlined in black and have a lighter color between them that forms a middorsal stripe. The stripe may be tan or greenish. There

are also broken parallel ridges on the dorsum. The tibia is approximately $\frac{3}{4}$ SVL. There is only a small amount of webbing at the base of the toes.

SIMILAR SPECIES: This species is similar to the *Ptychadena* species, but has only a very minimal amount of webbing. The extremely long toes are distinctive. There is still some disagreement regarding the species boundary between *S. fuelleborni* and *S. merumontanus* which some taxonomists consider to occur only on Mt. Meru.

HABITAT: Montane grasslands

NATURAL HISTORY: Breeding takes place in grassland streams. Eggs are laid under dense vegetation at the edges of streams and tadpoles hatch and develop in the water.

CALL: Pickersgill (2007) describes the call as “a breathy whistle, repeated singly or in sets of two or rarely three.”

DISTRIBUTION IN THE EACF: Mount Rungwe, Ufipa Plateau, and West Usambara, Uluguru, Rubeho, and Udzungwa Mountains.

TYPE LOCALITY: Poroto Mountains, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: 1500 – 3000 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ < 40 mm; ♀ < 53 mm

MAELEZO: Chura huyu ni mwembamba, ana miguu mirefu na vidole vya mguuni virefu sana. Pua imechongoka. Mstari mrefu mweusi unatoka puani hadi jichoni na unaendelea chini ya jicho, kupitia kiwambo cha sikio hadi mwanzoni mwa mkono. Mstari uliofifia unatoka chini ya jicho hadi mkononi chini ya mstari mweusi. Kuna matuta mawili mawili ya ngozi yanayoanzia nyuma ya jicho hadi kwenye tundu la kutolea haja na kutoa na kupokelea mbegu za uzazi. Matuta haya ni meusi na kati yao, kuna rangi iliyofifia ambayo inaunda mstari katikati ya sehemu ya juu. Mstari huo unaweza kuwa rangi ya hudhurungi au kijani kijani. Aidha, kuna matuta sambamba yaliyokatika kwenye sehemu ya juu. Miguu ni takribani $\frac{3}{4}$ ya SVL. Kuna utando kidogo sana mwanzoni mwa vidole vya mguuni.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: *Ptychadena*

MAZINGIRA: Nyika zilizopo 1200 m kutoka usawa wa bahari


HISTORIA ASILIA: Inazaliana kwenye vijito vya nyikani. Mayai yanatagwa kwenye uoto mnene pembeni mwa vijito; viluwiluwi wanatotolewa na kukua majini

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Milima Rungwe, Uwanda wa Ufipa, na Milima ya Usambara Magharibi, Uluguru, Rubeho, na Udzungwa.

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Milima ya Uporoto, Tanzania

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: 1500 – 3000 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Pyxicephalus edulis (Peters, 1854)

Lesser Bull-frog, Edible Bullfrog, Edible Frog



R. Drewes

SVL: ♂ < 100 mm; ♀ < 145 mm

DESCRIPTION: A large rotund frog with short legs. The dorsum is brown to green and covered in rough glands that are elongate or round. There are projections on the lower jaw that resemble teeth. The tympanum is small, but distinctly visible. The first finger is longer than the second. The toes are webbed only at the base.

SIMILAR SPECIES: Previously considered a subspecies of *P. adspersus*. The teeth-like projections and large size are distinctive.

HABITAT: Flooded grasslands and shrubland

NATURAL HISTORY: It is a fossorial species that is seen only in the rainy season. Breeding takes place in shallow pools with ample vegetation. Females lay several thousand eggs singly and scattered. Males guard tadpoles.

CALL: Described by Channing (2001) as sounding like “the barking of a small dog.

DISTRIBUTION IN THE EACF: Throughout the Eastern Arc Mountains and coastal forests of Kenya and Tanzania

TYPE LOCALITY: Tete, Mozambique

ELEVATIONAL RANGE: < 1500 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ < 100 mm; ♀ < 145 mm

MAELEZO: Chura huyu ni mkubwa, mviringo na ana miguu mifupi. Sehemu ya juu ni kahawia hadi kijani na ina tezi za kukwaruza ambazo ni ndefu ndefu na mviringo. Kwenye taya ya chini, kuna sehemu zilizojitokeza ambazo zinafanana na meno. Kiwambo cha sikio ni kidogo lakini kinaonekana. Kidole cha kwanza cha mkononi ni kirefu kuliko cha pili. Vidole vya mguuni vina utando mwanzoni tu.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Awali, ilidhaniwa kuwa spishi hii ni spishi ndogo ya *P. adspersus*. Spishi hii inatofautiana na zingine kwa sehemu zinazochomoza na kufanana na meno na saizi yake kubwa

MAZINGIRA: Nyika zilizofurika maji na maeneo ya vichaka

HISTORIA ASILIA: Spishi hii inachimba mashimo na kuishi chini ya ardhi na inaonekana tu msimu wa mvua. Inazaliana kwenye madimbwi yenye kina kifupi na uoto mwingi. Majike yanataga maelfu kadhaa ya mayai moja moja na yanatawanyika. Madume yanalinda viluwiluwi.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Maeneo yote ya MTMMP ya Tanzania na Kenya

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Tete, Mozambique

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: < 1500 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini.



Ranidae

The family Ranidae includes only one species found in the Eastern Arc and Coastal Forests. *Hylarana galamensis* is widespread, occurring across the savannas of eastern, central and western sub-Saharan Africa.

Familia ya Ranidae ina spishi moja tu inayopatikana MTMMP. Spishi hii ni *Hylarana galamensis* na inapatikana mahali pengi, kwenye maeneo ya savanna na mashariki, kati na magharibi mwa Afrika kusini mwa Sahara.



Hylarana galamensis
R. Drewes

Hylarana galamensis (Duméril and Bibron, 1841)

Marble-legged Frog, Golden-backed Frog, Galam White-lipped Frog



R. Drewes

SVL: ♂ 78mm; ♀ 86 mm

DESCRIPTION: The dorsum is glandular, with raised yellow-brown glands on smooth dark brown skin. There are broad, light dorsolateral folds. A pale ridge of skin runs across the upper lip from the tip of the snout to above the arm. There is a dark line above this ridge that runs from the nostril to the eye. The tympanum is visible, dark with white edges, and slightly smaller than the eye. The legs are short (tibia slightly less than ½ SVL) and stocky. There is at least one irregular dark horizontal line

on the tibia. Toe tips are not expanded. Toes are partially webbed.

SIMILAR SPECIES: The glandular texture of this species skin distinguishes it from similar species.

HABITAT: Permanent bodies of water in savannas; also common in towns

NATURAL HISTORY: Breeds in lakes and ponds and is seldom found far from permanent water. Females lay multiple clutches of over a thousand eggs. The eggs float on the surface of the water in a single layer.

CALL: Males call while floating in the water or from vegetation in the water. The call is described as “a nasal bleat” by Channing and Howell (2006).

DISTRIBUTION IN THE EACF: Coastal areas of Kenya and Tanzania, southern and western Tanzania and Mafia Island

TYPE LOCALITY: Senegal

ELEVATIONAL RANGE: < 900 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ 78mm; ♀ 86 mm

MAELEZO: Sehemu ya juu ina tezi za njano kahawia zilizoinuka, kwenye ngozi laini na kahawia iliyokolea. Kuna mikunjo ya ngozi mipana iliyofifia mgongoni na pembeni. Tuta moja la ngozi lenye rangi iliyofifia linapita kwenye mdomo wa juu, kutoka ncha ya pua hadi juu ya mkono. Kuna mstari mweusi juu ya tuta hili unaotoka kwenye tundu la pua hadi jichoni. Kiwambo cha sikio kinaonekana, ni cheusi, chenye weupe pembeni na ni kidogo kidogo kuliko jicho. Miguu ni mifupi (kidogo chini ya ½ ya SVL) na minene. Kuna angalau mstari mmoja wa mlalo bila mpangilio kwenye muundi goko. Ncha za vidole vya mguuni siyo pana na zina utando kiasi.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Ngozi ya spishi hii yenye tezi inaitofautisha na zingine zinazofanana nayo.

MAZINGIRA: Mkusanyiko wa kudumu wa maji kwenye savana, lakini pia inapatikana sana mijini.


HISTORIA ASILIA: Inazaliana kwenye maziwa na madimbwi na anapatikana kwa nadra mbali na maji ya kudumu. Majike yanataga makundi mengi yenye zaidi ya mayai 1,000. Mayai yanaelea juu ya maji yakiwa kwenye tabaka moja

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Pwani ya Kenya na Tanzania, Tanzania Kusini na Magharibi na kisiwa cha Mafia.

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Senegal

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: < 900 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Rhacophoridae

Rhacophoridae is primarily an Asian family, with only one genus, *Chiromantis*, occurring in Africa. Two species are found in the Eastern Arc and Coastal Forests. Both are large gray tree frogs with distinct disks on the fingers and toes. They build foam nests above water that protect their eggs until tadpoles hatch.

Vyura mchanga

Rhacophoridae ni familia ambayo kwa sehemu kubwa inapatikana bara la Asia; jenasi moja tu, *Chiromantis*, ndiyo inapatikana Afrika. Spishi mbili zinapatikana MTMMP; zote mbili zina vyura kijivu wakubwa sana wenye ncha butu za vidole vya mguuni na mkononi. Vyura hawa wanajenga viota vya povu juu ya maji ambavyo vinalinda mayai mpaka viluwiluwi vinapotokeza.



Chiromantis xerampelina
E. Harper

Chiromantis petersii (Boulenger, 1882)

Peters' Foam-nest Treefrog, Central Foam-nest Tree Frog



G.J. Measey

SVL: ♂ 37 – 44 mm; ♀ 50 – 53 mm

DESCRIPTION: Dorsum white to grey with prominent tubercles. The ventral surface is white. Males have a gray throat. The tympanum is distinctly visible. The eyes are large with horizontal pupils. The toes are expanded with small disks. The toes are extensively webbed with only one joint of the longest toe free of webbing.

SIMILAR SPECIES: Toes are not as extensively webbed as *C. xerampelina*. Toe disks are smaller than in *X. xerampelina*.

HABITAT: Dry savanna, shrubland and grassland. Can be found in agricultural and suburban areas as well.

NATURAL HISTORY: Foam nests are constructed by males whipping up secretions from their backs using their rear legs. The foam hardens on

vegetation overhanging temporary pools. Tadpoles hatch and drop in the water where they complete their development.

CALL: A series of quiet creaking croaks, sometimes repeated in short pulses.

DISTRIBUTION IN THE EACF: Inland areas of Tanzania and Kenya

TYPE LOCALITY: "Interior of East Africa"

ELEVATIONAL RANGE: < 1100 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ 37 – 44 mm; ♀ 50 – 53 mm

MAELEZO: Sehemu ya juu ni nyeupe hadi kijivu na ina sehemu ya ngozi ngumu iliyoinuka kwenye sehemu ya ndani ya mguu inayojitokeza. Sehemu ya chini ni nyeupe. Madume yana koo kijivu. Kiwambo cha sikio kinaonekana vizuri. Macho ni makubwa na yana mboni za mlalo. Vidole vya mguuni ni vipana na vina ncha ndogo mviringo. Vidole vya mguuni vina utando sana na kifundo kimoja tu cha kidole kirefu kuliko vyote hakina utando.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Vidole vya mguuni havina utando mwingi kama vya *C. xerampelina* na ncha mviringo za vidole ni ndogo zaidi pia.

MAZINGIRA: Savana kame, vichaka na nyika. Inapatikana pia kwenye maeneo ya kilimo na viunga vya miji


HISTORIA ASILIA: Madume yanatengeneza viota vya mapovu kwa kupiga majimaji yanayotoka mgongoni kwa miguu ya nyuma. Mapovu yanaganda kwenye uoto juu ya madimbwi ya muda. Viluwiluwi vinatolewa na kuanguka majini vinakokaa mpaka vikipata umbo kamili.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Maeneo ya bara ya Tanzania na Kenya

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: " Maeneo ya bara ya Afrika Mashariki"

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: < 1100 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Chiromantis xerampelina (Peters, 1854)
African Gray Treefrog, Foam Nest Treefrog



J. Vonesh

SVL: ♂ 43 – 75 mm; ♀ < 60 – 90 mm
DESCRIPTION: A slender gray treefrog, appearing almost completely white during the daytime. In some individuals the dorsum is mottled with a darker brown pattern resembling tree bark. The eyes are large with horizontal pupils, and the tympanum is distinctly visible. The fingers have wide expanded disks and are arranged in opposable pairs that wrap easily around small branches. Toes are completely webbed.

SIMILAR SPECIES: Toes are more extensively webbed than *C. petersii*. Toe disks are larger than in *C. petersii*.

HABITAT: Humid wooded savannas and semi-deciduous forests

NATURAL HISTORY: A single female and several males construct a foam nest on leaves or branches above water. The female must return to the pool several times during the construction of the nest to absorb enough water to complete the task. In some cases, she may even return the following night to add water to the nest. The large unpigmented eggs develop into small dark tadpoles which drop into the water after three to five days. The small tadpoles are only 18 mm in length.

CALL: Males call from vegetation above water. The call is described by Schiøtz as “subdued croaks and squeaks emitted irregularly.”

DISTRIBUTION IN THE EACF: Coastal Kenya and Tanzania and southern Tanzania. Also on the island of Zanzibar.

TYPE LOCALITY: Mozambique

ELEVATIONAL RANGE: < 1000 m

CONSERVATION STATUS: Least concern

UREFU WA MWILI: ♂ 43 – 75 mm; ♀ < 60 – 90 mm

MAELEZO: Amfibia minyoo huyu ni mwembamba, anaishi mitini na anaonekana karibu mweupe kabisa kutwa mzima. Katika baadhi ya vyura, sehemu ya juu ina madoa kahawia iliyokolea na mpangilio unaofanana na gome la mti. Macho ni makubwa, ana mboni mlalo na kiwambo cha sikio kinaonekana. Vidole vya mkononi vina ncha pana, mviringo na zimepangwa mbilimbili zikitazamana na kuweza kukamata vizuri kwenye matawi madogo. Vidole vya mguuni vina utando.

SPISHI INAZOFANANA NAZO: Spishi hii ina utando mwingi zaidi kuliko *C. petersii* na ncha mviringo za vidole ni vikubwa zaidi kuliko vya *C. petersii*.

MAZINGIRA: Savana yenye miombo na unyevu na misitu ambayo baadhi ya miti yake inaangusha majani yote wakati mmoja


HISTORIA ASILIA: Jike moja na madume kadhaa wanajenga kiota cha mapovu kwenye majani au matawi juu ya maji. Jike linarudi kwenye maji mara kadhaa wakati wa ujenzi wa kiota ili kuleta maji ya ujenzi. Wakati mwingine, linaweza hata likarudi usiku unaofuata kuongeza maji kwenye kiota. Mayai makubwa yasiyokuwa na rangi yanageuka viluwiluwi vidogo na vyeusi vinavyoanguka majini baada ya siku tatu hadi tano. Viluwiluwi ni vidogo na vina urefu wa 18 mm tu.

ENEO SPISHI INAPOPATIKANA KWENYE MTMMP: Pwani ya Kenya na Tanzania, kusini mwa Tanzania na kisiwa cha Zanzibar.

MAHALI KIELELEZO KILIPOPEWA JINA KWA MARA YA KWANZA: Msumbiji

ENEO LA SPISHI KUTOKA USAWA WA BAHARI: < 1000 m

HALI YA UHIFADHI: Haiko hatarini



Order Gymnophiona

Caecilians are elongate, limbless amphibians that are highly specialized for burrowing. Like frogs, they are carnivorous, eating most soil macroinvertebrates. The body is greatly elongate and segmented by annular grooves (folds in the skin) which may help them move through their burrows. Counting these primary annuli can help determine the species. The tail is short, but not present in any known African species. The eyes are small and covered with skin or bone. To the casual observer, they could be easily mistaken for earthworms.

Kabila la Amfibia minyoo

Caecilians ni vyura warefu sana, hawana miguu wala mikono na ni wachimbaji ardhi hodari sana. Kama vyura, wanakula wanyama na hasa karibu wanyama wote bila mti wa mgongo wanaoishi ardhini. Mwili ni mrefu sana na una mikunjo ya ngozi ambayo inajitokeza kama mistari inayozunguka mwili na inayougawanya katika sehemu ambazo zinawasaidia vyura kupita kwenye mashimo yao. Mistari hii inayozunguka mwili inaweza kusaidia kutofautisha spishi. Mkia ni mfupi lakini haupo kwenye spishi zozote za Afrika zinazojulikana. Macho ni madogo na yamefunikwa na ngozi na mifupa. Mtu asiye mtaalam anaweza kufikiri chura hawa ni minyoo.



Boulengerula niedeni
G.J. Measey

Caeciliidae

Boulengerula boulengeri (Tornier, 1896)

Usambara bluish-gray caecilian



G.J. Measey

SVL: ♂ 142 – 242 mm; ♀ 150 – 229 mm

DESCRIPTION: A pale blue to grey caecilian, darker above than below, from 80 to 250 mm in length. The mouth is recessed and the tail is absent. The heads of males are slightly larger than females, although the sexes are hard to tell apart in other ways. Oviductal eggs are visible through the skin of females. Primary annuli: 124 – 134.

SIMILAR SPECIES: The West Usambaras has a similar looking species.

HABITAT: It is a common species in the Usambaras and is found in the soil (typically the top 20 cm) in forests and on small-

farms. It is absent from compacted soils (e.g. tea plantations), but can penetrate very hard forest soils to depths > 50 cm.

NATURAL HISTORY: *B. boulengeri* lays eggs in a nest in moist soil that hatch directly into small pink caecilians. This species may have extended parental care with hatchlings feeding from the skin of their brooding mother, as reported for *B. taitana*. Eggs have been found in December and pink juveniles with their mothers during December and January, within the short rainy season. Adults are known to eat mostly termites and earthworms, but will take on most soil invertebrates which they find in their galleries, including large crickets which they spin to reduce the size so that it can fit into their mouths. Predators include the Usambara Garter Snake *Elapsoidea nigra*, which may predate solely upon caecilians. However, the most abundant predators are almost certainly invertebrates, including safari ants (*Dorylus molestus*).

DISTRIBUTION IN THE EACF: East and West Usambara (Channing & Howell 2006 recognize these animals as a different undescribed species. Details are likely to be very similar to the above) Mountains and on the Magrotto Ridge

TYPE LOCALITY: East Usambaras, Tanga, Tanzania

ELEVATIONAL RANGE: 300 – 1500 m

